ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 17 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Ris (kny: Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Suleiman Sarhan Said(Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma) Mwenyekiti Kamati ya Mawasiliano naUjenzi: Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati naomba kuweka mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano naUjenzi kuhusu Hotuba ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wiuzara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani mkiziangalia *order paper* zenu mtagundua kwamba hakuna maswali leo, ili tuweze sasa kumpa nafasi Mhe. Waziri aje asome Hotuba yake kwa kutulia, lakini maswali tutayaweka kesho yale ambayo tulikusudia yawepo leo, yangakuwepo leo kesho tusingekuwa na maswali kwa vile tungewaachia tu watu wachangie. Lakini pia mtagundua kwamba kesho ni siku ya Jumamosi na kwa mujibu wa kanuni ni siku ambayo sio siku ya kazi, lakini tumekubaliana kwamba kesho tuitumie.

Kwa maana hiyo nitamuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili aweze sasa kutoa hiyo hoja ili tutengue kanuni ili kutuwezesha kesho kutumia kama ni siku ya kazi kwa ajili ya michango kwa Wizara hii muhimu sana ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa sababu ya muda ulio mbele yetu hautoshi kutekeleza shughuli zote zilizo mbele yetu ili kwenda na wakati wa kukamilisha ratiba yetu ya baraza kama ilivyopangwa, na kwa kuwa kuanzia leo tutakuwa tuna hoja ya Wizara ya

Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, na kwa kuwa kama tunavyojua Wizara hii ni kubwa ina sekta nyingi, kwa vyovyote vile itakuwa na wachangiaji wengi na ili kutoa nafasi kwa wajumbe waweze kuchagia na kumpa nafasi Mhe. Waziri, kuweza kuja kufanya majumuisho kwa hivyo nilikuwa naliomba baraza lako tukufu tuweke kando kanuni ya muda ya 23.4 ili tuweze kutoa nafasi ya kufanya shughuli zetu kesho siku ya Jumamosi tarehe 18/6/2016 ili tupate nafasi nzuri ya kuchangia hotuba hii.

Mhe. Spika, kwa maelezo hayo naomba sasa kuliomba Baraza lako kwamba litengue kanuni ya muda tuweke kando ili tuweze kufanya shughuli zetu kesho siku ya Jumamosi kuanzia saa 3.00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana kwamba kesho siku ya Jumamosi tuje kazini kwa ajili ya kuendelea na michango ya Wizara hii wanyanyue mikono yao, wanaokaa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwe na kuafikiwa)

Mhe. Spika: kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kesho tutakuja kama kawaida saa 3.00 asubuhi na tutaendeleza shughuli zetu mpaka saa 9.00 mchana na kwa hivyo michango yote itakuwa kesho ili siku ya Jumatatu asubuhi Mhe. Waziri atakuja kujumuisha yale ambayo mtakuwa mmeyachangia kuanzia hiyo leo mpaka siku ya kesho, na itakuwa imekaa vizuri kwa sababu siku ya jumaapili itampa nafasi Mhe. Waziri kukaa na wataalam wake ili kuweza kupata majibu sahihi kwa hoja mbali mbali ambazo mtakuwa mmezitoa wakati wa michango yenu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi, Mawasiliano na Usaririshaji: Mhe. Spika,Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika,Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kukutana leo hii kuwasilisha na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kuniteua kushika dhamana ya kuiongoza na kuisimamia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Ni imani yangu kwa kushirikiana na watendaji wenzangu tutafanya kazi na kuhakikisha tunafikia malengo ya Wizara yaliokusudiwa.

Mhe. Spika, Napenda pia kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima katika kutekeleza majukumu mazito ya kitaifa. Aidha, naomba kumpongeza tena kwa dhati Makamo wa pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuongoza na kusimamia vyema shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, Napenda pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kushika nafasi ya uspika. Ni imani yangu kwa uzoefu wako ulionao utaliongoza na kuliendesha vyema Baraza hili kwa umahiri, hekima na busara hata wakati wakufanya maamuzi muhimu na magumu kwa maslahi ya nchi yetu. Aidha, pongezi zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika.

Mhe. Spika, Naomba nimalizie kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo kwa kazi nzuri ya uchambuzi wa kina wa taarifa za utekelezaji wa sekta na maelekezo na ushauri katika mpango wa bajeti ya Wizara ambao umeisaidia sana Wizara katika kukamilisha maandalizi ya bajeti tunayoiwasilisha.

Mhe. Spika, Serikali imeamua kufanya mabadiliko ya mfumo wa bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mabadiliko hayo ya mfumo wa bajeti yaliaza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 kutoka mfumo uliokuwepo unaotumia vifungu *(line item)* kwenda katika mfumo unaotumia programu *(Programme Based Budget - "PBB").*

Mhe. Spika, Bajeti hii ambayo naiwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu leo hii imeandaliwa katika mfumo wa programu kama Serikali ilivyoelekeza kwa kuzingatia utekelezaji wa Dira ya Zanzibar 2020, Mkakati wa Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii wa Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 -2020, Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar *(Zanzibar Transport Master Plan)* (2009), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, pamoja na maelekezo ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akizindua Baraza la tisa la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 05, Aprili, 2016.

B. TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2015 – MACHI, 2016 KWA KUTUMIA MFUMO WA PROGRAMU

Mhe. Spika,Taarifa hii ya utekelezaji ambayo ninaiwasilisha kwa kutumia mfumo wa programu unazihusu taasisi ambazo fedha zake ziliidhinishwa na Baraza la Wawakilishi - Zanzibar. Baada ya utangulizi huo, kwa heshima naomba uniruhusu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu kuu nne (4) za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kama ifuatavyo:-

B.1.PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA.

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri wa barabara zilizobora, salama na endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni uwepo wa miundombinu imara na huduma bora katika sekta ya Usafiri wa barabara.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara inasimamia programu ndogo mbili zifuatazo:-

(1a) Ujenzi na Matengenezo ya Barabara.
(1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara.

B.1.1 Programu Ndogo ya Kwanza: Ujenzi na Matengenezo ya Barabara.

Mhe. Spika,Programu hii ndogo inasimamiwa naIdara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara *(UUB)* ambayo imepewa jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara zote Unguja na Pemba ili ziweze kupitika muda wote.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni ukamilishaji wa km 30.2 za barabara ya Wete-Konde na Wete –Gando kwa kiwango cha lami. Aidha, Ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 53 Unguja na Pemba zinaendelea na kwa sasa barabara hizo zimefikia katika hatua mbambali za uwekaji wa kifusi. Barabara hizo ni Ole – Kengeja (km 35) na Barabara ya Jendele – Cheju – Kaebona (km 11.7) na Koani – Jumbi (km 6.3).

Aidha matengenezo makubwa ya barabara ya Ole – Konde kuanzia eneo la Meli tano hadi Chwale (km 13) kwa kufumuliwa, kuwekwa kifusi pamoja na lami yamekamilika.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya km 10.6 za barabara zimekamilika kwa kiwango cha kifusi, barabara hizo ni Wesha - Mkumbuu (km 2) , Pandani – Mlindo (km 2.6), Bumbwini – Kiongwe (km 4.3), na Barabara Ukongoroni ambayo inaunganisha na barabara ya *MIVARF* kuelekea Bwejuu (km 1.7).

Vilevile Matengenezo ya barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni yenye urefu wa (km 4) ambayo yanahusisha upanuzi wa barabara hiyo yanaendelea na hatua iliyofika kwa sasa ni kukamilika uwekaji wa kifusi kwa hatua mbambali pamoja na ujenzi wa kalvati, Mhe. Spika, niruhusu niongeze hapa kwamba uamuzi umekwishafanyika kwa barabara hiyo kuwekewa lami.

Mhe. Spika, Katika kipindi hicho, Wizara pia imekamilisha ujenzi wa barabara za ndani kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 5.5; barabara hizo ni Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka (km 1), Bungi – Muwembe kiwete (km 2.20), Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi (mita 400), Barabara inayoelekea Kiwanja cha magereza kupitia Mchina mwisho mpaka kituo cha afya Mpendae (km 1.5) na Barabara kutoka Chuo Kikuu Cha Sayansi Malindi hadi Malindi traffic (mita 460).

Vilevile, matengenezo mbali mbali ya kawaida ya barabara Unguja na Pemba yamefanyika kama vile uzibaji wa viraka. Aidha kazi za usafi wa barabara kama vile ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa misingi, madaraja na makalvati zimefanyika Unguja na Pemba. *KIAMBATANISHO NAMBA 4*

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 33,042,936,000 kati ya fedha hizo jumla ya TZS 31,595,725,000 ni kazi za maendeleo na jumla ya TZS 1,447,211,000 ni kwa

ajili ya kazi za kawaida. Mhe. Spika, wajumbe wa baraza lako tukufu wataona hapo kwamba fedha nyingi zimekwenda zaidi kwenye kazi za maenedeleo kuloko kwenye kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 8,688,130,340 zimepatikana, kati ya fedha hizo jumla ya TZS 7,719,140,940 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya sekta ya usafirishaji wa nchi kavu na jumla ya TZS 968,989,400 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

B.1.2 Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Usafiri wa Barabara.

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Usafiri na leseni ambayo imepewa jukumu la kusimamia usalama wa vyombo vya moto pamoja watumiaji wote wa Barabara, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto pamoja na kusimamia utoaji wa huduma za usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara. Aidha, jukumu jengine linalofanywa na programu hii ndogo ni kusimamia na kuendesha Karakana kuu ya Serikali iliopo Chumbuni na sehemu ya Mitambo ya Pemba.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni ukaguzi wa vyombo vya moto vya aina mbambali vipatavyo 24,296 Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa viko katika hali ya uzima na usalama. Aidha, jumla ya madereva wanafunzi 5,772 wamefanyiwa majaribio, waliofaulu 4,644 na waliofeli 1,086. Mhe. Spika, hao wanaosemekana kwamba wamefeli wanakwenda kupata mafunzo zaidi na watarejea na wengine huwa wanapasi. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya vyombo vya moto 388 vimefanyiwa matengenezo Unguja na Pemba. Vilevile, jumla ya ruhusa za njia 2026 kwa magari ya biashara aina mbali mbali zimetolewa Unguja na Pemba. KIAMBATANISHO NAMBA 5.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 577,732,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS 360,540,400 zimepatikana kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, Idara ya Usafiri na Leseni ambayo inatekeleza programu hii ndogo ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS.1,169,873,000 hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS. 670,346,500 zimekusanywa sawa na asilimia 57.3. Mhe. Spika, ni mategemeo yetu kwamba tukifikia tarehe 30 Juni, tutakuwa kamilisha asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu kuu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 33,620,668,000 na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya TZS 9,048,670,740 zilipatikana sawa na asilimia 27 ya makadirio ya bajeti.

PROGRAMU YA PILI: MIUNDOMBINU YA BANDARI NA VIWANJA VYA NDEGE

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya Ndege na Bandari. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma za usafiri wa baharini na anga. Aidha, programu hii inatekeleza lengo la kuwezesha ukuwaji wa sekta za uchumi kama vile sekta ya Biashara na Utalii.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege inasimamia programu ndogo mbili ambazo ni:-

(2a) Miundombinu ya Viwanja vya Ndege
(2b) Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri Baharini.

Programu Ndogo ya Kwanza: Miundombinu ya Viwanja vya Ndege

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la kupanga, kusimamia na kuratibu kazi za maendeleo katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni ukamilishaji wa kazi za uwekaji wa taa za kuongozea ndege wakati wa kutua na kuruka katika Uwanja cha Ndege wa Pemba. Aidha, ujenzi wa uzio wenye urefu (km 11.6) katika uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume umekamilika. Vilevile, Wizara kupitia programu hii inaendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal II) katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume ambalo limepitia katika hatua mbalimbali na linatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017 -2018.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 151,457,020,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 1,573,994,298 zimepatikana kugharamia miradi ya maendeleo ya sekta ya Usafirishaji wa Anga.

Programu Ndogo ya Pili: Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri Baharini.

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika

programu hii ndogo ni ukamilishaji wa ujenzi wa meli mpya ya abiria ya MV Mapinduzi II yenye uwezo wa kubeba abiria 1200 na tani 200 za mizigo ambayo imejengwa nchini Korea ya Kusini. Meli hiyo tayari imeshawasili Zanzibar na kuanza safari zake za kusafirisha abiria na mizigo kutoka na kwenda Unguja, Pemba na Dar es Salaam.Kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Serikali imeshawasilisha nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya mkopo. Aidha Benki ya Exim ya China inaendelea na tathimini ya mkopo huo na kwa nyakati tofauti wamekuwa wakihitaji kupatiwa ufafanuzi wa masuala mbalimbali.

Mhe. Spika**,** Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 900,000,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo kati ya fedha hizo jumla ya TZS 400,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na TZS 500,000,000 ni kwa ajili ya usimamizi wa huduma za usafiri Baharini. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 374,400,000 zimepatikana kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu kuu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 152,357,020,000 na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya TZS 1,948,394,298 zilipatikana sawa na asilimia 1.3 ya makadirio ya bajeti.

PROGRAMU YA TATU: HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).

Mhe. Spika, Lengo la programu hii ni kuhakikisha huduma bora na zenye kuendelea za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zinapatikana kwa muda wote hapa nchini. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa huduma bora za TEHAMA - Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inasimamia programu ndogo mbili ambazo ni:

(3a)Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano.
(3b)Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano.

Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano ambayo imepewa jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano pamoja na kuratibu uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano.

Mhe. Spika**,** Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kufanya matengenezo ya mkonga wa mawasiliano katika maeneo ambayo umeathirika na kwa sasa mkonga huo unafanya kazi kama unavyotakiwa. Aidha, jumla ya taasisi 54 tayari zinatumia huduma ya mkonga na taasisi 30 zipo katika hatua za mwisho za kuwekewa vifaa ili ziweze kutumia huduma hii. Vilevile, jumla ya minara ya mawasiliano ya simu 21 imejengwa na Kampuni mpya ya Halotel kutoka Vietnam ili kurahisisha mawasiliano ya simu na intanenti hapa Zanzibar.

Mhe. Spika**,** Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 84,646,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 25,305,400 zimepatikana.

Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano

Mhe. Spika**,** Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kutayarisha mpango mkakati wa miaka mitano wa mawasiliano Zanzibar pamoja na kutoa mafunzo kwa wakuu wa Mikoa na Wilaya zote za Pemba juu ya uelewa na matumizi ya mitambo ya mawasiliano picha "*video conference*" mitambo hii inawezesha kufanyika mawasiliano picha ya moja kwa moja baina ya watu walio katika maeneo tofauti Duniani. Mitambo hii hupelekea kupunguza gharama za safari sehemu ambapo mitambo hiyo imefungwa. Aidha walimu 76 wamefundishwa juu ya matumizi ya TEHAMA pamoja na matumizi ya mitandao katika kituo cha *ICT Community Center* cha Skuli ya Sekondari ya Kiembe Samaki.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 177,736,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 123,337,500 zimepatikana.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu kuu ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 262,382,000 na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya TZS 148,642,900 zilipatikana sawa na asilimia 56.7 ya makadirio ya bajeti.

PROGRAMU YA NNE: MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Spika, Progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha mipango bora na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni kuwepo mipango bora na uendeshaji mzuri

wa shughuli za utawala na utumishi katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Spika, Programu ya Mipango na Utawala ina programu ndogo tatu ambazo:-

(4a)Utawala na Uendeshaji;
(4b)Mipango na Sera katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirshaji;
(4c) Uratibu shughuli za Wizara Pemba

Programu Ndogo ya Kwanza: Utawala na Uendeshaji.
Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo imepewa jukumu la kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji katika Wizara.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kujenga uwezo wa wafanyakazi wapatao 42 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 10 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi. **KIAMBATANISHO NAMBA 3**.

Aidha, mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji yameimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi pamoja na stahiki zao.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 986,230,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 585,439,700 zimepatikana.

Programu Ndogo ya Pili: Mipango na Sera katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Spika**,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera na mipango pamoja na kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Spika**,** Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu mbambali za sekta ya Usafirishaji na Mawasilino, Uzinduzi (launching) wa mradi mkubwa wa mpango wa kuimarisha sekta ya Usafiri Tanzania kwa upande wa Zanzibar pamoja na kutoa mafunzo ya bajeti ya PBB kwa watendaji wa Wizara.

Mhe. Spika**,** Kwa mwaka wa fedha 2015 /2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 476,548,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo, hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 239,846,800 zimepatikana.

Programu Ndogo ya Tatu: Kuratibu shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa Ofisi Kuu – Pemba ambayo imepewa jukumu la uratibu wa kazi za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika**,** Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za Wizara Pemba ikiwemo kuratibu kazi za utawala na utumishi, kazi za mipango na bajeti, ujenzi wa barabara, huduma za usafiri wa barabara pamoja na huduma za TEHAMA.

Mhe. Spika**,** Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,405,852,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 851,096,900 zimepatikana.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 programu kuu ya Mipango na Utawala katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 2,868,630,000 na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya TZS 1,676,383,400 zilipatikana sawa na asilimia 58.4 ya makadirio ya bajeti. Maelezo kamili yamo katika **KIAMBATANISHO NAMBA 1**

TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA TAASISI NA MASHIRIKA YANAYOJITEGEMEA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea na kazi zake za msingi za kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali. Katika kipindi Julai 2015 hadi Machi 2016, Mamlaka imehudumia jumla ya safari za ndege 51,710 ikilinganishwa na safari 47,936 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2014/15 sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Kati ya safari hizo, safari za ndege 42,038 zilihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abedi Amani Karume na safari za ndege 9,672 zilihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Pemba. Kwa maelezo kamili tuangalie KIAMBATANISHO NAMBA 6.

Mhe. Spika**,** Aidha, Mamlaka imehudumia abiria 783,207 ikilinganishwa na abiria 744,381 katika kipindi kama hicho mwaka 2014/15 ikiwa ni ongezeko la aslimia 5.2. Abiria 705,046 walihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 78,161 walihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Pemba na abiria waliopita (*transit*) wamefikia 76,186. Kati ya abiria hao waliohudumiwa, abiria kutoka nje ya nchi walikuwa ni 386,432 kutoka abiria 307,495 katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia 25.7. Kwa maelezo zaidi angalia KIAMBATANISHO NAMBA 6.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa mizigo (*freight*) jumla ya Tani 1,397 zilihudumiwa katika viwanja vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na Tani 1,439 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai-Machi mwaka 2014/2015 ikiwa ni upungufu wa asilimia 2.9. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa safari za ndege za mizigo.

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 ilipanga kukusanya jumla ya TZS 5, 654, 719, 2675.654 na hadi Machi, 2016 jumla ya TZS 5,445,857,758.52 zimekusanywa

Malengo ya Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017, mamlaka inakusudia kutekeleza miradi ifuatayo: Utanuzi wa Eneo la Kuondokea na Kuwasili Abiria wa Kimataifa, Ujenzi wa *Business Centre*, Uimarishaji wa Ulinzi na Usalama wa Kiwanja cha AAKIA pamoja na Uwekaji wa Mfumo wa Kuwatambua Abiria.

Makadirio ya Bajeti Mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 mamlaka inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya TZS 9,790,780,648 kwa kazi za kawaida na kazi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo TZS 8,722,780,648 kwa kazi za kawaida na jumla ya TZS 1,068,000,000 kwa kazi za maendeleo.

C.2. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usalama wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo

vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama wa usafiri ndani ya maeneo ya bandari hizo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016, shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria katika bandari zake za Unguja na Pemba. Jumla ya meli za Kigeni 99 zenye uzito wa GRT 1,726,151 na meli za ndani 2,737 pamoja na vyombo vya kienyeji 2,755 zimehudumiwa. *KIAMBATANISHO NAMBA 7.*

Aidha, shirika limehudumia jumla ya tani 220,867 za mzigo mchanganyiko na tani 68,988 za mzigo wa majahazi pamoja na makontena 41762 (TEUs 52,938). Vile vile, jumla ya abiria 1,688,479 wa ndani na abiria wa nje 11,242 wamehudumiwa. *KIAMBATANISHO NAMBA 7*

Mhe. Spika, shirika limebadilisha maboya ya *solar* manne (4) katika Bandari ya Malindi na manne (4) katika Bandari za Pemba. Pia shirika limeyafanyia matengenezo maboya kumi na moja (11) katika Bandari za Pemba na kuunda maboya sita (6) Bubu kwa ajili ya Bandari za Unguja.

Mhe. Spika, kwa upande wa miradi ya shirika, shirika limenunua vifaa vya kufanyia kazi bandarini kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kuhudumia mizigo katika bandari zetu. Hadi kufikia Machi, 2016 shirika limetumia jumla ya TZS 5, 634, 580,998 kwa kulipia vifaa hivyo (Kreni 2, *Terminal Tractor* 2, *Trailler 2, Reach stacker 2, Fork Lift 3 na Empty Handler 1*) ambapo baadhi ya vifaa hivyo vimeshawasili. Kwa ujumla mradi huu unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 11, 035, 176,377.33. Kwa wale wanaotaka kuuliza kwa nini kuna senti 33 ni kwamba matumizi hayo yamepita kwa njia ya kibenki na huko benki wanavyotia riba zao wanafikia mpaka huko kwenye senti 33. Aidha, katika kuimarisha usalama wa vyombo vya baharini shirika limenunua maboya 7 mapya na taa 5 za *solar* za maboya ambayo yametumia jumla ya TZS. 448, 649,370.

Mhe. Spika, shirika limefanya matengnezo makubwa minara mitatu ya Chumbe, Makunduchi na Pungume ili kuimarisha miundombinu ya shirika. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS. 98, 287,686 zimetumika kwa ajili ya matengenezo hayo.

Aidha, shirika limelifanyia matengenezo banda la kukaa abiria wanaosafiri kupitia Bandari Kuu ya Malindi. Jumla ya TZS 335,241,071 zimetumika kwa ajili ya kazi hiyo pamoja na kuanza mradi wa matengenezo makubwa ya gati ya Wete.

Mhe. Spika, shirika limemalizia ujenzi wa gati ya Tumbatu. Hadi kufikia Machi, 2016, jumla ya TZS. 50,455,000 zimetumika kukamilisha ujenzi wa gati hiyo. Aidha, shirika linategemea kutekeleza ujenzi wa gati ya Mkokotoni kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, vile vile, shirika linaendelea na matengenezo ya eneo la kuwekea makontena katika Bandari ya Mkoani kwa kuweka uzio, taa pamoja na kuliweka sawa eneo hilo. Kazi hiyo inategemewa kutumia jumla ya TZS 34, 000,000.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai hadi kufikia Machi, 2016, shirika limekusanya jumla ya TZS 20,716,328,178 na kutumia jumla ya TZS13, 117,989,604 kwa kazi za kawaida.

Malengo ya Shirika kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, Shirika la Bandari linatarajia kutekeleza malengo mbali mbali katika utoaji wake wa huduma Bandarini Unguja na Pemba. Malengo hayo ni pamoja na kuhudumia jumla ya meli 177 za kigeni zenye uzito (*GRT*) wa tani milioni 2.56, meli za ndani zipatazo 4,040 na majahazi 4,025. Kuhudumia tani 311,355 za mzigo mchanganyiko, makontena 59,439(*TEUs* 76,062) pamoja na tani 96,452 za mzigo wa majahazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeo, shirika litafanya matengenezo makubwa ya Karakana ya kuwekea vifaa vya bandarini, manunuzi ya mikono ya kunyanyulia makontena (*Spreader*), kuimarisha kituo cha Kigomasha kwa kupeleka umeme na maji, kukamilisha matengenezo ya gati ya Wete pamoja na mradi wa kuimarisha ulinzi na usalama bandarini Malindi kwa kununua vifaa vya kuchunguzia mizigo ya abiria.

Makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, shirika limekadiria kukusanya jumla ya TZS. 29,895,185,266 katika kipindi cha mwaka 2016/2017 na limepanga kutumia jumla ya TZS. 23,780,022,201 kwa kazi za kawaida na TZS 9,877,779,987 kwa kazi za maendeleo.

C.3. SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR.

Mhe. Spika, Shirika la Meli na Uwakala limepewa jukumu la kuendesha meli zote za serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za kigeni

zinazoingia bandari za Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi 2016, shirika limeendelea kutoa huduma za uwakala wa meli zote za kigeni zinazoingia nchini kwa kutumia bandari zetu.

Mhe. Spika, shirika kupitia meli yake ya MV. Mapinduzi II limefanya safari 64 kwa kipindi cha miezi mitatu na jumla abiria 49,616 na mizigo tani 2,324 imehudumiwa ikiwemo magari na mizigo mengineyo.

Kwa upande wa MV. Maendeleo, jumla ya safari 34 zimefanyika na jumla ya abiria 22,241 na tani 4,950 za mizigo imehudumiwa. Kwa upande wa MT. Ukombozi, meli hii imekodishwa kwa Kampuni binafsi ya *GAPCO Zanzibar Ltd* kwa mkataba maalum.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi 2016, shirika limekusanya jumla ya TZS 5,259,144,776.95 sawa na asilimia 40 ya makisio ya mwaka na kutumia TZS 5,720,545,099.34 sawa na asilimia 46.

Makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 shirika linategemea kukusanya jumla ya TZS. 12,926,187,589 na kutumia jumla ya TZS 11,941,528,362.

C.4 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI.

Mhe. Spika, mamlaka ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli.

Kwa kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 mamlaka ilisajili meli 9 zenye uzito wa jumla *GRT* 5387 kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry*). Aidha, mamlaka kupitia ofisi yake ndogo ilioko Dubai ilisajili meli 87 zenye uzito wa jumla *GRT* 168,236. Kwa upande wa ukaguzi wa meli, Mamlaka ilikagua meli 29 ambazo ni sawa na *GT* 28,257. KIAMBATANISHO NAMBA 8.

Mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2015/16, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2,196,945,200 na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya TZS. 1,620,086,264 zimeapatikana na imetumia jumla ya T.ZS. 1,500,787,905.

Malengo ya Mamlaka kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, mamlaka itaendelea kuandaa na kuzipitia Sheria na Kanuni za Usafiri Baharini ili iweze kusimamia vyema makampuni na taasisi zinazotoa huduma katika Bandari za Zanzibar. Vile vile, mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano mzuri na imara uliopo baina yake na wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini pamoja na kutoa taaluma kwa wamiliki na watumiaji wa vyombo vya baharini. Mamlaka pia itaendelea kuimarisha usajili wa meli za kimataifa ili kuiongezea Mamlaka mapato pamoja na kuitangaza vyema bendera ya Tanzania.

Makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka imejipangia kukusanya TZS 3,642,689,600 na kutumia jumla ya TZS 3,492,378,460 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

C.5 SHIRIKA LA NYUMBA

Mhe. Spika, Shirika la Nyumba limepewa jukumu la kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusiana na ujenzi, uuzaji na ukodishaji wa nyumba za kuishi na za biashara.

Malengo ya Shirika la Nyumba kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, shirika linatarajia kuzifanyia matengenezo nyumba za shirika ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na kuwa katika hali ya usalama. Shirika pia lina lengo la kujenga nyumba mpya kwa ajili ya kukodisha na kuuza kwa taratibu maalumu.

Makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, shirika imejipangia kukusanya TZS 2,992,559,800 na kutumia jumla ya TZS 2,513,599,454 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

D. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya

Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Miongoni mwa Taasisi za Muungano tunazoshirikiana nazo ni:- Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (*TCAA*), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (*TMA*), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (*TCRA*), Shirika la Posta la Tanzania (*TPC*) na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Mashirikiano na Taasisi yamechangia sana kukuza Sekta ya Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

E. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyoelezwa katika utekelezaji wa kazi zetu kwa mwaka 2015/2016, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo zilisababisha utekelezaji wa baadhi ya kazi zetu kuwa mgumu. Changamoto hizo ni:-

- Uhaba na uchakavu wa zana zinazotumika katika ujenzi na utunzaji wa barabara;
- Kutokuridhiwa baadhi ya mikataba ya kimataifa kwa wakati kama vile" *Maritime labour Convention''* kunasababisha usumbufu katika usafiri wa baharini. Hata hivyo, hatua zinaendelea kuchukuliwa kwa ajili ya kutatua changamoto hii;
- Upungufu wa rasilimali fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- Kuharibika mara kwa mara vifaa vya kuhudumia Makontena Bandari ya Malindi kunatokana na uchakavu. Vifaa tayari vimeshagizwa na vinatarajia kufika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016 -2017. Mhe. Spika, ningependa kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba tunategemea vifaa hivyo kuwasili na kuanza kazi mwezi ujao wa Julai, 2016;
- Ukosefu wa vifaa vya kisasa na jengo la kufanyia ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa barabarani;
- Kutokuwepo kwa sheria na kanuni katika kusimamia huduma na miundombinu ya mawasiliano. Changamoto hii tayari inafanyiwa kazi na wizara.
- Utegemezi mkubwa wa washirika wa maendeleo katika kutekeleza miradi ya maendeleo;

- Ujenzi holela kwenye baadhi ya maeneo kumesababisha kutuwama kwa maji kwenye baadhi ya maeneo ya barabara zetu.

- Nyumba nyingi zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba zipo katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo makubwa.

F. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI BAJETI INAYOTUMIA MFUMO WA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na wizara pamoja na kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mamlaka na Mashirika yaliyo chini ya wizara kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016, sasa kwa ruhusa yako naombakuwasilisha bajeti inayotumia mfumo wa programu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Spika, Kufuatia mabadiliko ya muundo wa Wizara, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imepewa jukumu la kusimamia sekta ya Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji – Zanzibar. Hivyo kwa kuzingatia mabadiliko hayo, Wizara itakuwa na Programu kuu nne zifuatazo:-

Programu ya Kwanza: Miundombinu na Hudauma za Usafiri wa Barabara.
Programu ya Pili: Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa majengo ya Serikali na Binafsi.
Programu ya Tatu: Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).
Programu ya Nne: Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Spika, Kutokana na uhalisia wa majukumu ya Wizara katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, programu hizo zilizozitajwa hapo juu zitakua na programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:-

Programu ya Kwanza: Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara.
Programu ndogo (1a): Ujenzi na Matengenezo ya Barabara
Programu ndogo (1b): Usimamizi wa Usafiri wa Barabara
Programu ya Pili: Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa majengo ya Serikali na Binafsi

Programu ndogo (2a): Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi
Programu ndogo (2b): Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

Programu ya Tatu: Huduma za Teknolojia ya Habari na wasiliano (TEHAMA).Programu hizi nimekwisha zieleza kwa ukamilifu.
Programu ndogo (3a): Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Mawasiliano
Programu ya Nne: Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Spika, kuna programu nyengine ndogo ni:

Programu ndogo (4a): Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.
Programu ndogo (4b): Mipango na Sera katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.
Programu ndogo (4c): Uratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inatarajia kutumia jumla ya TZS188,554,100,000 kwa programu zote nne. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 157,150,000,000 ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya ujenzi wa Barabara na Viwanja vya ndege na jumla ya TZS 31,404,100,000 ni kutoka Serikalini ambapo jumla TZS 6,324,100,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya TZS 27,080,000,000 ni mchango wa Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara.

G. VIPAUMBELE VIKUU VITAKAVYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, napenda kugusia vipaumbele vikuu vitakavyotekelezwa na Wizara ya Ujenzi,Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 vimeweka vipaumbele vifuatavyo:

- Uendelezaji wa ujenzi wa Jengo jipya la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume.
- Kuanza ujenzi wa barabara ya Wete – Chake (km 22).

- Kuanza ujenzi wa barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni (km 31), Matemwe – Muyuni (km 7.6), Pale – Kiongele (km 4.6), na Fuoni – Kombeni (km 8.6).
- Kuanza ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri kwa awamu ya kwanza.
- Uendelezaji wa ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja (km 35).
- Ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Jendele – Cheju – Kaebona (km 11.7) na Koani – Jumbi (km 6.3).
- Ukamilishaji wa Upembuzi yakinifu wa mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

H. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU ZINAZOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, Programu kuu zilizotajwa hapo juu zimewekewa malengo mahususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbali mbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Maelezo ya programu na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

H.1 PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri wa barabara zilizobora, salama na endelevu. Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara ina programu ndogo mbili (2) ambazo ni; (1a) Ujenzi na Matengenezo ya Barabara na (1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara. Aidha, Programu hii inatekeleza lengo la Mkakati wa Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii wa Zanzibar la kuwezesha kupatikana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sekta mbali mbali Zanzibar.

H.1.1 Programu Ndogo ya Ujenzi na Matengenezo ya Barabara

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (1a) Ujenzi na Matengenezo ya Barabara. Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara ambayo ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara kwa kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya barabara na uwekaji wa miundombinu ya usalama barabarani. Orodha ya barabara zinazotarajiwa kufanyiwa matengenezo

makubwa kwa mwaka 2016/2017 kwa Unguja na Pemba zinaonekana katika KIAMBATANISHO NAMBA 4

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,244,538,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida. Gharama nyengine za programu hii ndogo ambazo zinahusu matengenezo ya barabara mbalimbali zinatoka Mfuko wa Barabara ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

H.1.2 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usafiri waBarabara

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara inasimamiwa na Idaraya Usafiri na Leseni ambayo ina lengo la kupatikana huduma bora za usafiri wa barabara zilizo salama kwa Unguja na Pemba. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ni usimamizi wa utoaji wa huduma za usafiri wa barabara, usimamizi wa usalama barabarani pamoja na matengenezo ya vyombo vya moto.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 561,430,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

H.2 PROGRAMU YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE NA UIMARISHAJI WA MAJENGO YA SERIKALI NA BINAFSI

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuwepo kwa makaazi bora yenye gharama nafuu kwa jamii pamoja kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe kihistoria na kiutamaduni. Programu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi ina programu ndogo mbili (2).

Programu hizo ndogo ni: Programu ndogo (2a) - Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi na
Programu ndogo (2b) - Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Aidha, programu hii inatekeleza lengo la Mkakati wa Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii wa Zanzibar la kutoa huduma za makaazi kwa wote.

H.2.1 Programu Ndogo ya Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (2a) Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi.

Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Ujenzi ambayo ina lengo la kuwepo kwa majengo bora ya Serikali na upatikanaji wa makaazi bora, salama na zenye gharama nafuu. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni uratibu na usimamizi wa shughuli za ujenzi; na usimamizi na matengenezo ya majengo.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 372,165,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

H.2.2 Programu Ndogo ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (2b) Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Programu hii ndogo inasimamiwa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ambayo ina lengo la kuhifadhi Mji Mkongwe na kuuendeleza kiutamaduni na kihistoria. Programu hii inatoa huduma ya usimamizi wa uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 360,900,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

H.3 PROGRAMU YA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO.

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora na zenye kuendelea za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zinapatikana kwa muda wote hapa nchini. Programu hii ina programu ndogo moja ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Mawasiliano. Aidha, programu hii inatekeleza lengo la Mkakati wa Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii wa Zanzibar wa kuwezesha kupatikana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sekta mbali mbali Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu ndogo hii ina lengo la kuhakiksha kuwepo kwa miundombinu na huduma endelevu za mawasiliano zilizo salama. Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, intanenti naposta, kusimamia upatikanaji wa huduma za TEHAMA kwa jamii pamoja na usimamizi wa miundombinu ya mawasiliano hapa Zanzibar.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 336,260,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

H.4 PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI.

Mheshimiwa Spika, Progamu ya Mipango na Utawala ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha mipango bora na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni (4a) Utawala na Uendeshaji, (4b). Mipango na Sera katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na (4c) Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

H.4.1 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (4a) Utawala na Uendeshaji. Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Programu hii ndogo inatoa huduma za kiutawala katika ofisi.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,022,331,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

H.4.2 Programu Ndogo ya Mipango na Sera katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (4b) Mipango na Sera katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo ina lengo la kuhakikisha mipango na sera mbali mbali za Sekta ya Usafiri na Mawasiliano inatayarishwa na kufuatilia utekelezaji wake. Huduma ambazo hutolewa katika programu hii ni kupanga, kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara, uimarishaji wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari pamoja na usimamizi wa usalama wa usafiri baharini. Miradi katika sekta ya usafiri wa Nchi kavu, Anga na Baharini ambayo itatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2016/2017 inaonekana katika KIAMBATANISHO NAMBA 2.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 183,198,666,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida na maendeleo.

H.4.3 Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya tatu - (4c) Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba. Programu hii ndogo inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo ina

lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika programu hii ni uratibu wa kazi za Wizara Pemba ikiwemo kusimamia shughuli za utawala na utumishi, mipango na bajeti, huduma za usafiri wa Barabarani, ujenzi wa majengo, huduma za TEHAMA pamoja na ujenzi na matengenezo ya Barabara mbali mbali – Pemba.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,457,810,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

I. HITIMISHO

Mhe. Spika, Kabla ya kumaliza hotuba yangu sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuendelea kutekeleza majukumu yake na kutatua changamoto mbali mbali zilizojitokeza katika kipindi kilichopita na hatimae kuipitisha bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Benki ya Exim ya China, Saudi Fund, Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazotoa Mafuta Duniani (OFID), UNESCO na wale wote wanaosaidia kutoa huduma za usafiri hapa nchini yakiwemo Mashirika ya Serikali na Binafsi kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuimarisha Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, Napenda kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum, Mwakilishi wa Jimbo la Malindi kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vile vile, nampongeza Katibu Mkuu Ndugu Mustafa Aboud Jumbe pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Shomari Omar Shomari, Wakurugenzi, Watendaji Wakuu wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ushirikiano na juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika; natoa shukurani kwa wadau wote wa Sekta ya Ujenzi, Mwasiliano na Usafirishaji pamoja na Makampuni na Mashirika mbali mbali ya ndani na

nje ya nchi yanayotoa huduma katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Michango ya Makampuni na Mashirika hayo yamesaidia sana katika kutoa huduma mbali mbali za usafiri, mawasiliano na ujenzi hapa Zanzibar. Shukurani za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wake wote kwa kuchapisha vizuri hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba pia nitoe shukurani zangu za dhati na za kipekee kwa familia yangu kwa kuniunga mkono na kunipa moyo muda wote katika kutekeleza majuku yangu ya kila siku.

J. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/ 2017.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya TZS 188,554,100,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2016/2017 kwa utekelezaji wa kazi zilizoainishwa katika programu nne za wizara ikiwa:-

- MatumizikwakazizakawaidakutokaSerikalinini**TZS 6,324,100,000.**
- MatumizikwakazizamaendeleokutokaSerikalinini**TZS 25,080,000,000.**
- MikopokutokakwaWashirikawaMaendeleoni**TZS 157,150,000,000.**

Mhe. Spika, hii inaonesha wazi kwamba katika wizara yetu fedha nyingi zimejikita kwenye kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Usafiri wa Barabara inayotekelezwa na Idara ya Usafiri na Leseni pamoja na Programu Kuu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa majengo ya Serikali na binafsi inayotekelezwa na Idara ya Ujenzi na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 1,762,800,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Unguja na Pemba kupitia huduma wanazozitoa.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo hayo ya TZS 1,762,800,000 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa uwasilishaji mzuri kabisa. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mheshimiwa na imeungwa mkono sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ili naye aje awasilishe hotuba yake. Katibu Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, Hotuba ya Maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kumalizika kwa kazi hii ya Kamati. Kwa kweli ushirikiano wao umetupa moya sana, na wameonyesha nia ya kuendeleza yale mazuri waliyoyakuta hapo wizarani na pia kuyaondoa yote yanayorejesha nyuma maendeleo ya wizara yao nasisi tunaahidi kufanyakazi nao kwa pamoja ili malengo waliyojiwekea yaweze kufikiwa.

Mhesimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukijadili na kupitia Bajeti hii, ambapo mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu na hatimae kujadiliwa na kupitishwa kwa lengo la kuiwezesha wizara kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka huu. Naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe pamoja na Makatibu wa Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Suleiman Sarahan Said	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
4.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	Mjumbe

5.	Mhe. Khadija Omar Kibano	Mjumbe
6.	Mhe. Mohammedraza Hassanaali	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
8.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
9.	Mhe. Said Omar Said	Mjumbe
10.	Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu
11.	Ndg. Himid Haji Choko	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa napenda nitoe Maoni ya Kamati kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni moja ya wizara muhimu katika nchi yetu kutokana na ukweli kwamba inasimamia sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, ambazo ni Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Usafiri wa Baharini, Sekta ya Usafiri wa Anga, Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu pamoja na Sekta ya Mawasiliano. Aidha, baada ya maelezo hayo naomba sasa niaze na uchambuzi wa Programu zinazosimamiwa na wizara hii.

PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

Mhe. Spika, kamati yangu imepata nafasi ya kufanya ziara ya siku mbili Unguja na Pemba kabla ya kuipitia Bajet hii ya mwaka 2016/17, pamoja na ufinyu huo wa muda kamati ilijifunza mambo mengi ambayo ni changamoto za wizara na kwa kweli iko haja ya kuweka mipango madhubuti ili kuhakikisha kazi za wizara zinaenda kwa kasi kwa mujibu walivyojipangia wao bila ya vikwazo vyovyote. Aidha, kamati yangu imejipanga kuisaidia sana wizara katika kipindi chote ambacho Mhe Spika umetutuma tuisimamie. Pamoja na hayo, kamati yangu imeipitia Bajeti hii katika mazingira magumu haswa ukizingatia Wajumbe wangu wengi ni wageni hapa Barazani lakini pia hawajawahi kuikagua wizara nzima pamoja na kukutana na wafanyakazi ili kujua changamoto zao ili kamati ikaweza kuisaida wizara ipasavyo. Lakini pamoja na hayo nawashukuru Wajumbe wangu kwa umahiri wao jinsi walivyoweza kutoa michango yao kwa wizara kupitia uzoefu wao na msaada mkubwa wa watendaji wao wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hii, lakini naamini mwakani wataweza kuisaidia sana wizara ili kuona changamoto zao zinageuka kua chachu ya maendeleo kwao.

Mhe. Spika, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa

Barabara mbili kati ya tatu kwa upande wa Pemba zenye urefu wa kilomita 30.2. Barabara hizo ni barabara ya Wete - Konde na Wete - Gando na bado barabara moja ya Wete -Chake. Kwa kweli kukamilika kwa Mradi huu kunaondoa ile adha ya usafiri iliyokuwa ikiwakabili wananchi wanaotumia barabara hizo.

Mhe. Spika, kamati yangu imetembelea Mradi huo na kushuhudia wenyewe kazi kubwa iliyofanywa na Kampuni ya *Mwananchi Engineering and Contracting Co. Limited (MECCO)*, iliyopewa Kandarasi ya kujenga barabara hizo. Kwa kweli barabara hizo zimejengwa kwa kiwango kinachohitajika haswa kwa wakati huu tulionao. Kamati inaamini kwamba serikali haikufanya makosa kuiteuwa Kampuni ya *MECCO* kuipa kazi hii, kwani kiwango cha ubora wa barabara hizo ni kikubwa sana na cha kupigiwa mfano kwa hapa Zanzibar. Pamoja na mafanikio hayo, lakini bado kuna barabara hii ya Wete – Chake ambayo ni sehemu moja ya barabara hizo haijaanza kujengwa hadi leo, ili kukamilisha mradi huo wa barabara tatu za Pemba kutokana na Serikali kuchelewa kutoa pesa za fidia wananchi ambazo zinakadiriwa kufikia karibu Bilioni moja na milioni mia saba (1.7 Bil), ambazo zingelimuwezesha mjenzi kuendelea na kazi hiyo iliyobakia.

Kwakweli suala hili limeisikitisha sana Kamati yangu kwani kutokana kuchelewa kwa mradi huu kunaweza kuongeza gharama za mradi huo kuliko bajeti iliyopangwa hasa kutokana na gharama za vifaa kupanda bei siku hadi siku, lakini baada ya kuangalia Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka huu wa 2016/17 tumeziona pesa hizo 1.7 Bilioni zimetengwa kwenye bajeti hiyo ili kumalizia malipo hayo ya fidia kwa wananchi ili mjenzi aendelee na kazi iliyobaki ya kukamilisha bara bara hiyo ya Wete-Chake.

Mhe. Spika, kamati yangu inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuipatia wizara pesa hizo mara tu baada ya kuipitisha bajeti hii kwani sio kwamba ikishalipwa fidia kua kazi hiyo itaanza hapohapo, kwani hapo kutakua na kazi za kuanza kuondoa baadhi ya nyumba na vipando mbali mbali vilivyomo katika eneo la mradi kazi ambayo pia itachukua muda. Kwa hiyo, kutolewa mapema kwa pesa hizo kutaharakisha ukamilishaji wa ujenzi huo ambao umeshakua wa muda mrefu ambao uliasisiwa tangu mwaka 2009.

Mhe. Spika, hivyo kamati yangu kwa masikitiko kabisa, inakujuiilisha kwamba bado Kampuni hiyo ya *MECCO* licha ya kuing'arisha Pemba kwa ujenzi wa barabara hizo, bado haijakamilishiwa malipo ya kazi hiyo ya kujenga barabara hizo. Ambapo kampuni hiyo inadai karibu USD 3 milioni na Tshs 1.7 wakati kazi wameshamaliza zaidi ya miaka mitatu nyuma, jambo ambalo

linaisababishia serikali kujiongezea mzigo wa madeni pamoja na riba ya ucheleweshaji wa malipo ya mradi (*Interest*), ambapo mzigo huo huwabebesha wananchi bila sababu yoyote.

Mhe. Spika, lakini pamoja na hayo tunamshukuru Mhe Waziri kwa kuiahidi kamati kua suala hilo limeshafika ofisini kwake na ameshalitolea maelekezo ufanyike uhakiki wa madai hayo na mwenye haki yake apewe. Hii imetupa moyo kamati jambo ambalo limekwama kwa muda zaidi ya miaka mitatu waziri ameahidi kulitatua kwa wakati muwafaka ili kazi zisikwame kwa sababu zisizo za msingi.

Mhe. Spika, kutokana na kadhia hii ya ucheleweshaji wa malipo hasa kwa pesa zinazotoka kwa wafadhili. Kamati yangu tunamshauri Waziri wa Fedha kuwateua maafisa katika kila mradi ili kuwepo wizarani kwa muda wote wa mradi ili kuona na kujua changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwasilisha Wizara ya Fedha ili kuondoa usumbufu wakati wa malipo, kwani imeonyesha wakati mwingine kunatokea kutokufahamiana kwa baadhi ya watendaji baina Wizara ya Fedha yaani mlipaji **(***PAYEE***)** na wizara yaani mwenye mali **(***CLIENT***),** ambapo jambo hili tunaona sio sahihi kwani hao wote ni watendaji wa serikali na wanafanya kazi ya wananchi kwa maendeleo yetu sote sio ya mtu fulani. Aidha, tatizo hili sio kwa wizara hii tu, bali ni kwa miradi yote inayopatiwa pesa kutoka kwa wahisani au mikopo ya nje. Wizara ilipojipangia malengo ya mwaka mmoja basi huhitaji watekeleze kama walivyopanga na kusiwe na vikwazo, hasa kwa utaratibu wa sasa wa Bajeti inayozingatia Program (*PBB*) maana yake mipango iende kwa wakati.

Mhe. Spika, aidha, juhudi za serikali za kuwasogezea maendeleo wananchi wake, ilijenga barabara tano za ndani za Mkoa wa Kaskazini Pemba chini ya Ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation (MCC-T)* na kazi hii ilipewa Kampuni ya H. Young ya Kenya. Ujenzi wa barabara hizo zilizojengwa kwa kiwango cha lami kwa urefu wa kilomita 35 ambao ulijumuisha barabara za Kipangani - Kangagani, Chwale – Kojani, Mzambarau Takao - Pandani hadi Finya, Mzambarau Karim – Mapofu, Bahanasa – Daya na Makoongeni – Mtambwe.

Mhe. Spika, kamati yangu ilibahatika kuzitembelea barabara hizo na kugundua changamoto kadhaa zikiwemo dosari zilizojitokeza muda mfupi tu, baada ya kukamilika ujenzi wa barabara hizo mara tu baada ya kukabidhiwa kwa serikali. Dosari hizo pia pamoja na nyufa na mmong'onyoko wa udongo katika sehemu mbali mbali za barabara hizo. Aidha, kamati yangu imegundua kwamba baada ya kusikiliza ushauri wa jopo la wataalamu, mwajiri *(MCC-T)*

pamoja na wizara kwa ujumla waliamua kufanyika kwa matengenezo kadhaa ili kuzihami barabara hizo na kazi hii ilikabidhiwa tena kwa Kampuni ya *MECCO* kwa gharama ya Dola za Kimarekani Milioni 1.68.

Mhe. Spika, kamati yangu baada ya kuona changamoto kwenye barabara hizo tunaishauri serikali kabla ya hizi kampuni hasa za ujenzi wa Barabara kuzipa kazi za ujenzi *(TENDER)* basi ni vyema zile *tender board* kuangalia vizuri vigezo *(B.O.Q)* pia na uzoefu wa kazi na kujiridhisha kwa kuona kazi zilizofanywa na kampuni hizo na sio kuja kujifundishia kazi hapa kwetu. Mhe. Spika, kwani pesa zinazotumika ni pesa za wananchi hivyo zinapaswa kutumika vizuri.

Mhe. Spika, hili nnalisema kwa uzoefu. Mhe. Rais wetu wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. (JOHN POMBE MAGUFULI) wakati akiwa Waziri wa Miundombinu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kuwafukuza kazi wakandarasi wasiokuwa na viwango na pia kukataa kuzipokea barabara ambazo zilikuwa zimejengwa chini ya kiwango. Hii imemjengea sana sifa wakati huo na ndio maana wananchi wanamkubali kwa umakini wake na umahiri wake wa kutokua na muhali wakati anapokua kazini na hadi hii leo amekuwa Raisi bora Duniani na kila pahala amekuwa akisifika.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri wetu tunamuomba aige mfano wa Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli asikubali kuipokea kazi ambayo itakakuwa chini ya kiwango na pia asiikubali Kampuni yoyote ambayo haina uzoefu wa kufanya kazi na kuja kujifundishia kwenye wizara yake, kwani ndani ya wizara yake huko nyuma zipo Kampuni zilipewa kazi zikashindwa njiani na nyingine zimekimbia na hadi leo kazi zimelala na kurejesha nyuma maendeleo ya nchi yetu na ukiangalia historia za kampuni hizo ni zile zilizoletwa na wajanja kwa tama zao na kuitia hasara serikali**.** Vile vile, kamati yangu itamsaidia kumpa nguvu pale atakapoamua kuifukuza kazi kampuni yeyote ya mkobani.

Mhe. Spika, nchi nyingi za kiafrika zinakabiliwa sana na changamoto hii ya kujengewa barabara zilizo chini ya kiwango na kuzibebesha mzigo serikali zao, kwa hili sisi hatutolikubali.

Mhe. Spika, pia, kamati yangu ilishitushwa sana na kiwango cha pesa nyingi zilizolipwa kwa fidia kwenye ujenzi wa barabara hizi za Pemba karibu Tshs. 6 Bilioni kiwango hiki ni kikubwa sana, ambapo kamati ilipoiuliza wizara wakasema haikuhusishwa na ulipaji wa fidia hizo. Suala hili kwa kua kamati haijakusudia kuundwa kwa kamati teule kulifuatilia suala hili tunaitaka wizara ilifanyie kazi na ituletee ripoti kamili ya uhakika na uhalali wa malipo hayo

kwani ukiangalia katika maeneo hayo hakuna majumba mengi kiasi hicho ambapo gharama ingekua kubwa kiasi hicho. Kwani kama hatukua makini hasa kwenye masuala ya fidia basi miradi itakua na gharama mara mbili ya bajeti halisi kutokana na ukubwa wa fidia hizo zinazotolewa, nasema haya kwani hadi hii leo bado kuna malalamiko ya wananchi kuhusu fidia hizo.

Mhe. Spika, hadi kamati yangu inapitia bajeti ya wizara hii, kazi hii ya marekebisho ya barabara hizo ilikua inaendelea ingawa kulikua na madai ya kujitokeza vipingamizi kadhaa kama vile idara zenye dhamana ya rasilimali zisizohamishika kutoa pingamizi ya kuchimba na kusafirisha kifusi na mawe kwenda eneo la kazi. Kutokana na suala hili tunaziomba taasisi zote za serikali kutoa mashirikano wakati wa kutekeleza miradi bila ya kujali mradi unatekelezwa wizara gani kwani zote ni taasisi za serikali hiyo, tofauti ni mgawanyo wa majukumu tu.

Mhe.Spika, kutokana na kadhia hii na nyenginezo zinazofanana na hii, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa utekelezaji wa Miradi Mikubwa kama hii, kuna umuhimu mkubwa wa kuwashirikisha mapema kabisa wataalamu wa ndani pamoja na watunzaji na waendeshaji wa Miradi hiyo itakapomalizika ili kujikinga na hasara na usumbufu unaoweza kujitokeza baada ya kukamilika kwa Miradi hiyo.

Mhe. Spika, vile vile, Kamati yangu inazidi kuipongeza Serikali, kupitia Wizara hii kwa kuendelea na juhudi zake za kutatua kero za wananchi katika sekta hii ya usafiri wa nchi kavu, hususan kuanza kwa Ujenzi wa Barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni pamoja na sehemu mbali mbali kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Waziri iliyomalizika hivi punde inaonyesha kwamba ujenzi wa Barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni umefikia hatua ya uwekaji wa kifusi kwa hatua mbali mbali pamoja na Ujenzi wa *Culvert*.

Mhe. Spika,Kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi ninayoiongoza, imepata bahati ya kukagua mradi huu na hadi tunaondoka katika sehemu hiyo barabara ilikua inasubiri utiwaji wa lami ili mradi uweze kukamilika kabisa. Hata hivyo, shughuli ya uwekaji wa lami bado ilikua ni kitendawili kisichokuwa na jawabu kutokana na kukosekana na ruhusa kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika, Kamati imegundua kwamba barabara hii inajengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Barabara, ambapo kwa mujibu wa Mkataba wa Ujenzi wa Mradi huu Kampuni ya *MECCO* ilitakiwa kuifanya kazi hadi hatua hii ya Kifusi tu, na

baadae kazi ya utiaji wa lami ifanywe na Idara ya Utengenezaji na Utunzaji wa Barabara Serikalini, lakini kutokana na uhalisia uliopo na kwa kuaangalia uwezo wa Kampuni hii ya Kizalendo ya *MECCO*, kumekuwa na mazungumzo na mwelekeo wa kuitumia tena Kampuni hii kwa kazi za utiaji wa lami. Pia, Kamati iliarifiwa kwamba bado taasisi zinazohusika hazijatoa baraka za kukabidhiwa na kuanza shughuli hiyo kwa Kampuni ya *MECCO*.

Mhe. Spika, kwa kuwa kila mmoja wetu anafahamu umuhimu wa Barabara hii, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inaiomba Serikali kufanya maamuzi ya haraka "ikibidi kukata pua kujenga Wajihi" ili kazi za utiaji wa lami katika barabara hii iweze kukamilika na kuanza kwani imeshapitwa na muda. Hata hivyo, **(***PBB***)** kuendelea kubaki kama ilivyo hivi sasa kazi iliyokwisha kufanyika inaweza kuharibika kwa kuchimbika kwa kifusi kilichowekwa. Vile vile, kuendelea kucheleweshe utiaji wa lami katika barabara hii, kunaendelea kuleta adha na athari kubwa kwa wananchi waishio pembezoni mwa barabara hiyo kutokana na mavumbi jambo ambalo licha kuharibu afya zao inasumbua hadi kwenye mapishi yao wanakula vumbi usiku na mchana adha kwa watumiaji pamoja na wananchi wanaishi pembezoni mwake kuendelea kuteseka kiafya na kimazingira.

Mhe. Spika, Kamati yangu imegundua changamoto kubwa mbili katika mradi huu, moja na hatua ya utiaji wa lami, ni nani atakaetia lami na nyingine ni miundombinu ya mabomba makubwa ya maji yuliyoko kwenye barabara hiyo ambapo kamati yangu ilijitahidi kusaidiana na wizara hii ya Miundombinu kuwakutanisha na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tunawashukuru Mawaziri wa Wizara hizi mbili pamoja na manaibu wao pamoja na Mwenyekiti wa Mfuko wa Barabara kwa mashirikiano waliyoyatoa kwa Kamati ili kukwamua tatizo hilo na walituahidi katika kikao hicho kulitatua suala hilo kwa haraka ili kazi iweze kuendelea, tunaitaka Bodi ya Mfuko wa Barabara kutoa fedha kwa haraka ili mradi ukamilike, mara nyingi tumekua tukilalamika kuchelewa kwa miradi kutokana na kuchelewa pesa kutoka kwa wahisani lakini leo cha kushangaza huu mfuko wa Barabara ni pesa ya Serikali yenyewe pia inakosekana kupatikana kwa wakati na kusababisha mradi kukwama bila ya sababu za msingi, nadhani Mhe Waziri akija atatusaidia wajumbe ni hatua gani imeshafikiwa katika kuondoa changamoto hizo ili mradi ukamilike.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe.Waziri ajitahidi kuwasimamia watendaji wake ili kuikamilisha Barabara hiyo ya fuoni kwasababu Serikali imekua ikisemwa sana na wananchi kwa kadhia ya barabara hiyo badala ya kusifiwa kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara hizo jambo ambalo halipendezi kwa

Kamati yetu na naamini hata kwa Waziri mwenyewe, na kwa moyo aliotuonyesha kwa muda mfupi tulipoanza kufanya kazi nae tumemuona ni kiongozi makini na ana nia ya kuondoa changamoto za Wizara kwa muda mfupi sana.(*Makofi*)

PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwaendeleza wananchi wake na pamoja na jitihada zake za kuimarisha huduma mbali mbali za Kijamii, Kitaifa na Kimataifa. Bado, kuna haja ya kujitathmini, kujiridhisha na kuwa makini kabisa wakati wa kuingia Mikataba ya Miradi mikubwa ya kimaendeleo. Kwa kweli, utafiti na upembuzi yakinifu pamoja na ushirikishwaji wa wadau ni vitu vya msingi ambavyo vinaweza kusaidia wakati wa uwanzishwaji wa Miradi hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu imekagua Ujenzi wa Jengo jipya la Abiria *(Terminal 2)* katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Kwa kweli malalamiko na manung'niko mengi kuhusiana na kutoridhishwa na mwenendo na utekelezaji wa Mradi huu. Ujenzi wa Mradi huu umekuwa ukizungumzwa kwa muda mrefu sasa, sio tu na Wajumbe wa Baraza lako tukufu, bali pia na watalamu mbali mbali wa majego pamoja na wadau wa masuala ya usafiri wa Anga.

Mhe. Spika, Kamati yangu imegundua kwamba, kulikua na mapungufu kadhaa katika mchoro wa awali ikiwemo maegesho ya ndege kuwa karibu mno na jengo la abiria pamoja na njia ya kurukia ndege *(Run way)* kuwa juu kuliko jengo lenyewe, jambo ambalo linaweza kuleta usumbufu na uharibifu mkubwa wa mali na vifaa hapo baadae wakati wa mvua kubwa kama hazijachukuliwa hatua za dharura ikiwemo kujenga mtaro wa kutolea maji ya mvua ili kuondoa tatizo hilo, pamoja na Kamati yangu kuambiwa kuwa mtaro utajengwa na kuyapeleka maji kwenye bwawa la kuhifadhia maji ya mvua lakini kamati yangu haijaridhika na hatua hiyo kwani inaonyesha itakua ni hatua ya dharura bali tunashauri uwepo mradi mwingine maalum kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wa kuyatoa maji ya mvua uwanjani kuyapeleka hadi pwani (Baharini). Hiyo ndio itakua ufumbuzi wa kudumu kwa kuyaondoa maji ya mvua hapo uwanjani.

Mhe. Spika, kutokana na chanagamoto hizo, Kamati haikuridhika na mwenendo mzima wa Mradi huu, Mradi ambao awali ulianza kwa dola za Kimarekani 70,400,000 (2009) na kufanyiwa marekebisho (June 2012) kwa kuongezwa Dola 11,828,674.71 na hatimae Aprili, 2014 ulifanyiwa

marekebisho mengine na kuongezwa tena Dola 46,518,414.80 na kufanya jumla kuu kufikia Dola za Kimarenani 128,747,089.51**.** Hiki ni kiwango kikubwa sana cha fedha kwa mradi mmoja jambo ambalo sisi wajumbe tangu ulipoanza mradi huu tulianza kutilia mashaka jinsi ya ushirikishwaji wa wadau mbali mbali jambo ambalo lilitawaliwa na manung'uniko miongoni mwa watendaji wa Serikali na hata Wajumbe kuzuia Bajeti kutokana na kizungumkuti cha mwenendo wa mradi huu, pamoja na hayo lakini Kamati yangu inamtaka Mhe. Waziri kuwa jasiri na makini zaidi na kuangalia changamoto hizo lakini cha msingi sasa tunataka mradi ukamilike na tuanze kuutumia kwa maslahi ya taifa.

Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe.Waziri, kuisimamia miradi ya Wizara kwa karibu zaidi kwani tumeona karibu miradi yote ya Wizara hii imekua ikiongezeka gharama zake kila siku ukiangalia hili sio jambo la kudharau hata kidogo.

Mhe. Spika, jambo jengine katika Mradi huu wa *(Terminal 2)* ni changamoto ya kutokushirikishwa kwa wadau mbali mbali ambao watakaoutumia Uwanja huo tokea mwanzo, lakini pamoja na hayo Kamati yangu inaitaka Wizara kuhakikisha inaitisha vikao mbali mbali vitakavyowashirikisha wadau wote ikiwemo Mamlaka yenyewe ambayo ndio watakaokuja kukabidhiwa jengo hilo ili kuanza kupanga ni namna gani wataweza kuja kuutumia na kuudhibiti uwanja huo, changamoto nyingine kamati yangu iliyoiona ni kiwango kikubwa cha Umeme kitakachokuja kutumika katika kuendeshea kiwanja hicho na utaratibu wa mapato na matumizi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege baina yao na Wizara ya fedha, na hili ni vyema katika hivyo vikao vyao tunavyowashauri Wizara basi na hili muanze kulizingatia mapema ili kuepuka usumbufu hapo baadae.

Pia Kamati yangu inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuliekea kinga ya Bima ya ajali ya moto jengo hilo kwani ni jengo la gharama kubwa kwa hiyo ni vyema kuliekea tahadhari mapema, kwani mfano mzuri hivi karibuni katika nchi jiraji ya Kenya kiwanja cha *JomoKenyatta Airport* kiliungua moto lakini kwa kua kiwanja kimekatiwa Bima basi kiliweza kukarabatiwa kwa muda mfupi na kuendelea na kazi kama kawaida, lakini pia kwakua kiwanja kitatumika na wageni mbali mbali pamoja ndege kubwa za kimataifa basi ni lazima kiwanja kiwahahakikishie wadau wote wataokitumia kuwa kiko katika hali ya usalama mkubwa wakati wote.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kitabu cha Mhe. Waziri pia kinaonyesha kupungua kwa Tani za Mizigo iliyohudumiwa kwa mwaka huu, ambapo walihudumia Tani 1,397

ikilinganishwa na Tani 1,439 mwaka jana kwa madai ya kupungua kwa idadi ya ndege maalum za Mizigo. Kamati inaomba kupatiwa maelezo ya kina juu ya mapungufu haya na namna ya Mamlaka ilivyojipanga kukabiliana na tatizo hilo kwani tunategemea kila kiwanja kinavyoboreka basi iendane na makusanyo yatakavyoongezeka.

Mhe. Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Pemba, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kukamilisha Mradi wa Utiaji wa Taa za Kuongozea Ndege wakati wa kutua na kuruka katika kiwanja hicho. Hata hivyo, Kamati haijaridhika na matumizi ya kiwanja hicho kwani hadi hivi sasa hakuna ndege yoyote inayotua ama kuruka baada ya jua kuzama. Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, hali hii inakuja kutokana na kwamba Makampuni yanayotoa Huduma za Usafiri wa ndege kuleta ndege zenye Injini na propela moja tu, ambazo haziruhusiwi kuruka baada ya jua kuzama. Kutokana na kadhia hii, Kamati inachukuwa fursa hii kuiomba Serikali kuwashajihisha watu wa Kampuni za ndege kuleta ndege ambazo zinaweza kutoa huduma hata baada ya jua kuzama. Aidha, Kamati pia inasisitiza juu ya uimarishwaji wa usafi pamoja na vitendea kazi katika Uwanja wa ndege wa Pemba kwani hali ilivyo hivi sasa bado haiiridhishi.

Pia Kamati yangu imepata taarifa tangu taa hizo kutiwa hapo kiwanjani basi hakuna ndege iliyowahi kwenda huko usiku, kwa hiyo bado tunashauri Wizara kuhakikisha kila inapokusudia kufanya maboresho katika maeneo yake basi ni vyema kuwashirikisha wadau ili kuweza kupata ushauri wa uwekaji wa miundombinu na kupata matokeo mazuri wakati wa matumizi ya miradi yao. Ndio maana tukasema hata huo uwanja Mkubwa basi washirikishwe wadau wote ikiwemo Mamlaka yenyewe na taasisi binafsi zitakazokuja kuutumia uwanja huo, kwani hata sekta binafsi zinamawazo mazuri ya kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege na maeneo mengine.

Pia kamati yangu inaishauri Serikali isione taabu kuingia mikataba ya (PPP) katika kuundesha uwanja wa Ndege Terminal 2 kwani utahitaji uangalizi wa hali ya juu na maarifa makubwa ya kuuendesha uwanja huo, lakini pia kwa kuzingatia matumizi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kupewa heshima zao maalum kwenye mikataba hiyo. Kwani Uwanja huo ni mali ya Umma.

PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO NA SERA KATIKA SEKTA YA UJENZI, USAFIRI MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Spika, Kamati yangu inalipongeza sana Shirika la Bandari kwa kazi nzuri za kutoa huduma za kuzihudumia Bandari zetu za Unguja na Pemba, pamoja na

changamoto za ubaba wa fedha za kununulia vifaa vya kisasa katika kuendeshea kazi zao, Kamati ilipokea maelezo kua wakati mwingine inapohitaji mkopo kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar inabidi kutumia pesa zao za ndani jambo ambalo linarejesha nyuma Shirika letu. Kutokana na taarifa hiyo, Kamati yangu inamuomba Waziri kupitia Katibu wake Mkuu ambae ni mzoefu wa masuala ya Bandari kulisaidia Shirika kupata fedha hizo na ikiwa kuna ugumu kwa *PBZ* Basi wasiogope kwenda kwenye mabenki mengine kukopa ili kujiimarisha kihuduma na kibiashara, kwani kwa mujibu wa Sheria ya Shirika wanayohaki ya kukopa, kushtaki na kushtakiwa, kwa hiyo suala la fedha kisiwe kikwazo cha kukwamisha shughuli zao.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari ni lango kuu la kuingilia mizigo yote hapa Zanzibar kutoka nchi za nje, lakini bado Bandari zetu zina mapungufu makubwa sana katika vitandea kazi hasa *Crane* za kisasa ambazo zingeliweza kupakua mizigo kwa haraka, lakini pia Shirika lina changamoto kubwa ya mahala pa kuhifadhia Makontena. Jambo ambalo pia husababisha usumbufu mkubwa wa msongamano hapo Bandarini, kwani pale kwenye uwanja wa Hoteli ya Bwawani yalipokua yakihifadhiwa hivi sasa eneo hilo haliwezi kutumika tena, kwa hiyo tunalitaka Shirika kutafuta eneo jingine mbadala la kuhifadhia makontena ili kuondoa usumbufu kwa wafanya biashara wenye makontena.

Mhe. Spika, namuomba Mhe.Waziri akija aje kutusaidia ufafanuzi hivi karibuni kampuni moja ya meli *CMC* inayoleta Makontena hapa Zanzibar walitoa *circular* kwa wateja wao kua kunaongezeko la karibu USD 200 kwa Kontena kutokana na *conjestion* ya Makontena hapo Bandarini, je suala hili ni kweli? Na kama ni kweli je, Shirika limechukua hatua gani kuihami hali hiyo.Kwani ongezeko ya bei ya usafirishaji pia huathiri bei za bidhaaa hapa Zanzibar**.**

Mhe. Spika, pia, Kamati yangu inaipongeza Serikali kupitia Shirika la Bandari kwa ujenzi wa Gati ya Tumbatu lakini inaiomba Serikali kwenye Bandari ya Mkokotoni kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti mizigo na abiria wanaoingia pale kwani kuna mapato mengi ya kodi ya Serikali hayakusanywi na pia kuna watu huingia kiholela kupitia Bandari hiyo.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Kamati yangu haijapata nafasi ya kuitembelea Bandari ya Pemba lakini tunaishauri Wizara kupitia Shirika kutafuta *Crane* kubwa katika Bandari ya Pemba kwani inaleta usumbufu mkubwa hasa kunapotokea mizigo mikubwa pale Bandarini. Pia, Kamati yangu inalitaka Shirika kuangalia uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wavuvi huko kwenye mnara wa matumbini ili usije kuleta athari kwa mnara ule.

Mhe. Spika, Kamati inachukua fursa hii tena kuipongeza Serikali kwa kwa kusikia kilio cha Wajumbe wa Baraza lako tukufu lililopita kwa kuitaka Serikali kununua Meli yake ya kubeba abiria na mizigo hasa baada ya kuona ajali za baharini zimekua nyingi na za kutisha kutokana na upungufu wa vyombo vya usafiri wa Baharini jambo ambalo lilipoteza maisha ya wananchi wengi pamoja na mali zao kwa mashirikiano na kuliomba Baraza kuruhusu kukata matumizi ya viburudishaji na vinywaji kwenye bajeti za Wizara na tukaweza kufunga mikanda na leo tunajivunia kua tumeweza kununua meli ya MV. Mapinduzi II. ambayo hivi sasa inaendelea na safari zake kama kawaida. Hata hivyo, kumekuwa na taarifa tofauti kuhusiana na upakiaji wa Mizigo ndani ya meli hiyo, inasemekana hivi sasa meli hiyo inashindwa kupakia baadhi ya mizigo ikiwemo magari.

Kutokana na taarifa hizo, Kamati inahitaji Maelezo ya kina juu ya kadhia hiyo. Vile vile, Kamati inashauri kuangaliwa upya kwa utaratibu wa ukusanyaji wa mapato ya meli hii kwani kunataarifa kwamba wanaosimamia meli hii sio wanaokusanya mapato hayo, jambo ambalo Kamati yangu haijafurahishwa nalo kwani inaweza kuleta usumbufu mkubwa hasa katika kuihudumia Meli hiyo. Kamati yangu inaitaka Wizara kuwaekea misingi watendaji wa Shirika, ili kuweza kudhibiti mapato yake na pia kutumia kufuatana na taratibu za Shirika zinavyosema ili kuhakikisha Meli hiyo inakua safi, na kutoa huduma bora kwa wananchi kama inavyotarajiwa.(*Makofi*)

PROGRAMU YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE NA UIMARISHAJI WA MAJENGO YA SERIKALI NA BINAFSI

Mhe. Spika, Shirika la Nyumba imepandisha kodi ya nyumba kutoka shilingi 25,000/= kwa mwezi hadi shilingi 75,000/=. Kiwango hiki ni kikubwa ukizingati kwamba wengi wa wapangaji hao ni wa kipato cha chini. Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na watendaji wa Shirika hilo ili kufikiria upya mabadiliko hayo kulingana na vipato vya wananchi wetu, pamoja tunajua kua Shirika linahitaji kujitegemea lakini pia tufikirie na wengi ya wanaoishi ni wananchi wenye kipato cha chini, tunashauri kupandisha kodi kwa ghafla kwa asilimia 150 sio jambo sahihi kuzingatia hali ya watu wetu, isipokua kwa zile nyumba zinazotumika kibiashara kama maduka, mikahawa na biashara nyengine hizo wangeliweza kuwapandishiwa kodi kiasi hicho au hata zaidi**.**

Mhe. Spika, Kamati yangu inaelewa mzigo mkubwa uliokabidhiwa Shirika la nyumba kuanzishwa likiwa na nyumba karibu zote zimeshachakaa na zinahitaji mtaji mkubwa ili kuzirejesha katika ubora wake wa asili na ukarabati huo

unahitaji pesa nyingi tungeliishauri Serikali kulipatia mtaji Shirika hilo ili kutafuta nguvu za kujitegemea kibiashara na kutoa huduma za makaazi, vyenginevyo kuwabebesha mzigo huo kwa ghafla wananchi wetu kwakweli sio sahihi na huo ni mtihani wetu sote. Pia tunalishauri Shirika hilo kubuni miradi kwa kushirikiana na taasisi za fedha za ndani na nje ili kujenga majengo kwa ubia na wateja mbali mbali ili kuweza kujenga majumba ya kisasa na kuweka miji yetu katika sura nzuri kama inavyotakiwa. Kamati yangu pia inalitaka Shirika kuzifanyia ukarabati nyumba za maendeleo zilizojengwa na uongozi wa awamu ya kwanza kwani baadhi yao hivi sasa zimeanza kuhatarisha maisha yao, vilevile kamati yangu inataka Shirika lipige marufuku wale wapangaji wote kwenye nyumba za maendeleo kuacha mara moja kuzivunja nyumba hizo na kutia milango ya nyuma na milango ya biashara bila kushirikisha Shirika lenyewe kwani hupelekea kusababisha kupunguza uimara wa majengo hayo, kwani wengine hufanya *Saloon*, milango ya nyuma n.k.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe ni moja ya miji ya urithi wa kimataifa, na ni hazina kubwa Mwenyeenzi Mungu aliyotujaalia, mji huu umekua ni sehemu moja ya vivutio vya wageni kuja kutembelea Zanzibar. Mji huu umekua ukiipatia nchi yetu mapato mengi ya pesa za kigeni, lakini pia wasomi wengi wa historia wamekua wakija kuutembelea na kufanya *research* zao kupitia Mji Mkongwe wa Zanzibar. Mji huu umehifadhi majengo makongwe ya kihistoria, ambapo yalijengwa karne nyingi zilizopita, kwa hivyo, ni mji ambao unaopaswa kuhifadhiwa, kulindwa na kudumishwa na Wazanzibari sote, ili kulinda hazina hiyo. Kwa nchi za wenzetu kama vile Misri imekua ni moja ya kiingizio kikubwa cha mapato kwa nchi zao, kutokana na kuvitangaza vivutio vyao vya kihistoria, ikiwemo majengo na rasilimali zilizomo kama kumbukumbu za matukio ya nchi zao.

Mhe. Spika, kamati yangu inaitaka Mamlaka kupitia Mhe. Waziri, wamejipanga vipi kuuhifadhi mji huo, hasa kutokana na ujenzi wa majumba mengi ya kisasa yanayojengwa katika mji huo ambayo hayaendani na uasilia wa majengo hayo. Lakini isitoshe kamati yangu inaendelea kusikitishwa sana na kuona kuwa jengo la Mji Mkongwe limefikia hali ya kuanguka sehemu ya jengo hilo na hadi leo limeshindwa kukarabatiwa. Pia, kamati yangu inataka majibu kutoka kwa waziri. Je, fedha zinazopatikana kutokana na jengo hilo zinadhibitiwa na taasisi gani? Kama kuna taasisi inayokusanya mapato ya hapo ilikuaje hadi jengo kufika kubomoka bila kufanyiwa ukarabati kwa wakati. Pia, kamati yangu inaitaka wizara kuhakikisha jengo hili linakarabatiwa na kulirudisha katika hali yake ya kawaida.

Mhe. Spika, pia, kamati yangu inataka kujua katika Mji Mkongwe, kuna majumba mangapi yanayohifadhiwa, pia je, yako majengo katika Mji Mkongwe hayamo katika uhifadhi. Je, kwa kuwa kuna idadi kubwa ya nyumba za Mji Mkongwe ambazo zimechakaa na hazifai kuishi binadamu kwa usalama wao, lakini bado nyumba hizo zinaendelea kuishi watu. Je, ni hatua gani za kisheria zinachukuliwa, ili kunusuru maisha yao, na kama ikitokezea nyumba kuanguka na kuathiri maisha yao, je, Mamlaka ya Mji Mkongwe inawajibika vipi?

Mhe. Spika, kabla sijamalizia hotuba yangu, napenda sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu. Pia, napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Bajeti ya Wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chake Chake, naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wachangie na wakosoe na kushauri pale penye kasoro, ili ikipita iwe bajeti yetu sote na tumpe nguvu waziri wetu msikivu, kwenda kuyatekeleza yale tuliyomuelekeza na yale aliyotuomba tumkubalie akayatekeleze kwa maslahi ya wananchi wetu na Taifa letu kwa ujumla. Hatimae nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote wa Baraza hili tukufu kuunga mkono Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii, kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti Mhe. Hamza Hassan Juma, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, na mimi naomba dakika tano kidogo nitoe maoni yangu kabisa. Nakushukuru sana Mhe. Spika, nawashukuru na wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi, mawaziri, manaibu mawaziri, viti maalum, wabunge wa majimbo nawashukuru sana.

Mhe. Spika, na mimi nataka nitowe angalizo la kwanza kwenye meli yetu ya Mapinduzi. Mhe. Spika, kwanza nataka niseme maneno ambayo yanaletwa kwenye mitandao yetu sio ya kweli, meli yetu haijasusiwa, wananchi wetu wa Pemba wanapanda na bado meli yetu haijasusiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, inawezekana hii ni *propaganda* ya kibiashara au ni *propaganda* nyengine, lakini meli inapandwa na watu na mapato yanaendelea kama kawaida. Isipokuwa namshauri Mhe. Waziri, kwamba kweli meli yetu kama nilivyozungumza kuna upungufu wa kupakia mizigo. Kwa kweli meli yetu ina *style* ya kama ile *land craft* ya Jitihada ya kufika juu, na kwa kule Pemba meli ile haina sehemu ya kutosha, iko sehemu ndogo ambayo inafanya. Kwa hivyo, ningeishauri wizara ikahakikisha kwamba meli yetu kule Pemba inafunga gati hiyo ambayo inatakiwa kwa kushusha magari. Meli yetu ina uwezo mkubwa tu wa kuchukua gari kiusalama zaidi. Hilo ningeliomba zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kwa ajili ya kamati yangu. Nataka niwatowe wasi wasi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa barabara ambazo zinajengwa kwa kiwango cha lami, ambapo wajitayarishe wananchi bila kusikia *propaganda* ni barabara ya Donge Mwanda, Kinduni - Kitope, Kijitoupele - Nyarugusu - Fuoni Mambosasa, barabara ya Ole - Kengeja, Hospitali ya Chake Chake - Tibirinzi, Mwanakwerekwe - Fuoni na Mgagadu - Kiwani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kidogo kuhusu barabara hii ya Mwanakwerekwe Fuoni kwa niaba ya kamati yangu, mimi nataka niwatowe wasi wasi wananchi wote na wajumbe wa Baraza letu la Wawakilishi. Mhe. Spika, barabara hii kwa mambo tulivyokwishayapanga, kama nilivyoeleza. Kamati ilishafanya jitihada kubwa ya kuzikusanyisha wizara zote pamoja na mfuko wa barabara. Kuna maneno sijui barabara ya Kimarekani itajengwa na Mmarekani. Hii inajengwa na Mfuko wa Barabara, nataka niwatowe wasi wasi na kwa taarifa pesa zake zipo na panapomajaaliwa ninachowaomba wananchi wote wawe na stahamala, kitu kizuri kinakuja ndani ya mwezi wa saba, barabara ile itaanza kutiwa lami. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, nataka niwatowe hofu watu wenye barabara ya Wete - Chake Chake, Mkoani - Chake Chake, barabara hizi nakuhakikishia katika kipindi hiki tukijaaliwa zikimaliza barabara zile, basi na hizi nazo zinafuatia. Pia, nataka niseme wananchi wangu wale wanaolilia barabara ya Msingini, basi wakae mkao wa kula kwa barabara hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niiombe kamati kwamba barabara ya Kengeja - Mtambile, barabara hii ilijengwa kwa nguvu za *UUB*, lakini barabara hii kidogo inahitaji matengenezo ya ziada, waifanyie ukarabati kabla haijaanza kukosa muelekeo.

Mhe. Spika, vile vile, nataka niwatowe wasi wasi wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu na wananchi, kwamba *Terminal II* tukijaaliwa tutahakikisha

katika kipindi hiki cha miaka miwili basi *Terminal II* tutaitumia tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, nataka niseme Shirika la Nyumba, nasema kwamba nakubali na naipongeza serikali kwa kuunda shirika hili. Lakini Mhe. Spika, kwa upeo mkubwa nataka tuangalie vitu viwili vya kuvienzi na vyengine vya kufanya. Mhe. Spika, shirika nalikubalia linataka lijiendeshe kibiashara. Mwanzo shirika hili lilianza na shilingi moja, likaja na shilingi moja na nusu, likaenda na shilingi tatu, likaenda na shilingi tano, shilingi tisa, shilingi 21, kwa kipindi cha shilingi 21 na kuanzia shilingi 25 katika kipindi cha miezi mitatu imeshapita zaidi ya asilimia 300 kupandishwa. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme kuwa wizara yangu hii ya mawasiliano, nitowe mfano. Sikatai nyumba sasa hivi zina mashiko makubwa, lakini nataka niangalie vya kutosha, nyinyi ni mashahidi. Kuna nyumba ambazo ziko Kengeja hata mtu ukimpa bure hazitaki. Leo unazipandisha hizi 75 atakaa nani. Kuna nyumba ziko Micheweni ukimpa mtu bure basi hataki kukaa, kuna nyumba ziko Bambi ukimpa bure mtu hataki kukaa. Kuna nyumba ziko Gamba ukimpa bure mtu hataki kukaa.

Mhe. Spika, ningeiomba Shirika la Nyumba, sikatai kodi, lakini angalau ingekuwa isizidi shilingi 25,000, na kwa kodi hii ningeomba kwa sababu ya kumuenzi huyo aliyetoa kwa nia safi ya nyumba hizi, baadae tukijenga nyumba nyengine kila mtu ana hiyari yake, lakini mule tujuwe tumewatafuta masikini tukawavunjia vibanda na kuwaweka mule. Kwa hivyo, ningeshauri kwa nyumba zile tukawatoza na kodi ambayo inastahili. Hilo napenda kuliwasilisha.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza zaidi ni kuhusu masuala ya uongo. Mhe. Spika, kweli Pemba kuna tatizo dogo sana tena ninavyotaka kuzungumza ni kwamba wasitajwe Wapemba...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Namalizia tu, Mhe. Spika. Wasitajwe Wapemba. Wako waswalihina, wako waliokuwa safi, wako wenye imani na wako wa aina tofauti. Anayefanya vitendo Mhe. Spika, basi anafanya kwa ridhaa yake na kwa uchungu wake na kwa ufisadi wake basi. Lakini Mhe. Spika, tusitaje Wapemba na mimi nimo sijafanya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeshauri wasitaje Wapemba, anayefanya kitu afanye kwa niaba yake na serikali itachukua mkondo wake. Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chake Chake, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa uwasilishaji wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tuna matangazo machache kabla hatujaanza kuchangia. Kwanza ni tangazo la wageni. Wageni waliopo leo ni wageni wa Mhe Abdalla Maulid Diwani, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Jang'ombe, ni viongozi wa Jumuiya ya Kupambana na Changamoto za Vijana na Mazingira, jumla yao ni wanane na wanaongozwa na Katibu wao ndugu Ali Mohamed Haji, naomba mnyanyuke popote pale mlipo. Ahsanteni sana na karibuni kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine linatoka kwa Mwenyekiti wa Uwawaza, anawatangazia kwamba baada ya kumaliza kikao anawaomba Waheshimiwa Wajumbe wanawake wote wabakie.

Baada ya hao Waheshimiwa Wajumbe, mpaka sasa wachangiaji ambao wameshaomba ni 30 na wanaendelea, kwa sababu bado karatasi zinakuja. Lakini leo tutapata nafasi za wajumbe watatu tu kwa mujibu wa wakati tulionao.Labda niwataje kabisa ili wajifahamu.

Kwanza kabisa kwa heshima na taadhima atachangia Mhe. Zulfa Mmaka Omar, na kwa upendeleo nitampa Mhe. Ali Salum Haji Kirova, na mwisho atakuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo labda niseme kwamba kesho wajumbe mlio wengi mtapata kuchangia, na tumekuwa na utaratibu wa kuakhirisha maswali ili kuwapa nafasi wajumbe wengi zaidi kuchangia. Lakini leo tuliondosha maswali tukasema sasa tuyaweke kesho, kwa maana kwamba yatazidi pia kubana nafasi za watu kuchangia. Kwa hivyo, mtatuwia radhi kwa wale ambao mtakosa nafasi kwa siku ya kesho, kwa sababu tunakusudia yale maswali ambayo yalikuwayaje leo basi yaje kesho. Au tunaweza tukaamua vyenginevyo baada ya kutoka hapa, pia tukayaakhirisha maswali ili kukupeni nafasi zaidi. *(Makofi)*

Baada ya maelezo machache hayo sasa naomba kwa heshima na taadhima nimwite Mhe. Zulfa Mmaka Omar, ili aweze kuanza kuchangia. Mhe. Zulfa Mmaka, tafadhali. *(Makofi)*

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo ya upendeleo kuchangia katika wizara hii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kuisoma vizuri hotuba hii, ndani yake muna mambo mazuri, manjonjo, tumshukuru. Pia, nimpongeze Mhe. Suleiman Sarahan Said maarufu 'Jembe', kwa kufanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nilishtuka nilifikiria kwamba ni Naibu Waziri, kumbe ni mtu wa kamati, hongera sana kwa kuitetea wizara yangu hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara hii mimi nishukuru kwamba ndio wizara iliyonilea katika maadili mazuri hadi kufikia leo Mhe. Zulfa Mmaka Omar, kuniona kwamba nafaa kuwa kiongozi. Niishukuru wizara hii kwa kunilea katika maadili mazuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nianze kuchangia na kilio changu kinakuja katika *stand* ya magari. Mhe. Spika, Chake Chake tunakilio cha *stand* ya magari na kilio hiki kimeshakuwa ni kikubwa kila siku tunakileta hapa. Mimi katika hotuba hii leo nilijua kwamba changamoto ya mwanzo tutakayotengenezewa nilijua ni ile *stand* ya magari ya Chake Chake.

Mhe. Waziri, wewe ni mgeni katika wizara hii, lakini nikuambie kwamba Chake Chake tuna tatizo la *stand*. Chake Chake tuna matatizo ya maegesho ya magari; Magari kutoka Wete, Mkoani na Micheweni yote yanakutana katika *stand* iliopo Chake Chake, ambapo *stand* hiyo ni ndogo na ni finyu. *Stand* ile hata magari 30 ukiyapanga mule hamutoshi.

Pia, katika mji wa Chake Chake maegesho ya magari yamekuwa ni tabu sana. Utakuta kuanzia Madungu hadi Chachaani, pembeni ya barabara unakuta magari yamejipanga ovyo ovyo na ambayo hayana utaratibu maalum. Kwa hivyo, hiyo inaleta tatizo, tungekuomba Mhe. Waziri, utakapokuja na majumuisho yako utueleze ni lini tatizo letu la *stand* ya Chake Chake utalimaliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikitoka hapo kwenye *stand*, nije katika Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni ni sehemu ambayo inaingiza mapato mengi serikali yetu. Lakini Mhe. Spika, idara hii Pemba imesahauliwa na nasema hivi kwa sababu idara hii jengo lake kwa Pemba sio zuri, tulikuwa na jengo bovu pale, *Alhamdulillah* tunashukuru *UUB* walituhurumia na kutugaiya kijengo chao kile, lakini lile jengo Mhe. Spika, halitoshi kwa sababu ni ndogo sana.

Mhe. Spika, jengo hilo ambalo limetolewa sasa hivi lina takribani miezi isiyopungua saba au nane halina mafeni, wala *AC*, kwa sababu lile jengo ni la viyoo, kwa kweli unapata uhatarishi wa maisha ya wafanyakazi waliomo mule, ukizingatia kwamba ofisi ile inahudumikia watu kutoka nje, ina makonda, ina madereva na ina wafanyakazi wengine wanaokuja kutoka mawizarani, lakini la kusikitisha zaidi ni kwamba jengo lile halina ubora wa kuwahudumia wale watu, inahatarisha hali za wafanyakazi Mhe. Spika.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri, anieleze ni lini jengo lile la kugaiwa utalifanyia ukarabati ili wafanyakazi wale waweze kufanyakazi katika mazingira mazuri. Pia, ile idara ni kubwa kwa Pemba, lakini hakuna gari hata moja katika idara ile. Utakuta idara ile inatakiwa kwenda kufanyakazi nje kwenda kukagua magari yaliyopata ajali, kwenda kufanya ukaguzi wa shaka, kwenda kutafuta madereva ambao wanafanya makosa. Lakini utakuwa kwamba tumewapa kazi nzito, lakini hatujawapa kitu ambacho kitawafanya wao wafanye kazi zao kwa uaminifu. Idara ile watu wote wanatumia magari yao. Wengine hawana magari, inabidi wewe unamfuata dereva kafanya tatizo, halafu unapanda katika gari ya abiria haileti sura nzuri. Kwa kweli lile ambalo limekusudiwa haliwezi kupatikana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri, katika pesa zake hizo angetenga japo kidogo, wapate japo Kirava *Four* kidogo kwa ajili ya kwenda kutembea kwenye kazi zao, ili na wao wajuwe kwamba hizi kazi tulizopewa tumeshapewa nyenzo ya kwenda kufanyia kazi. Naamini kwa uzuri wako wa kazi hiyo gari sijui kama kesho haitopelekwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije kwenye sehemu ya mitambo. Mhe. Spika, Pemba tuna sehemu ya mitambo lakini imebakia jina tu sehemu ya mitambo. Pale pahali hapana kitu chochote cha kuitwa kwamba ni sehemu ya mitambo Pemba, unaweza kwenda ukaambiwa spana hakuna, unataka kuziba mipira unaweza kuambiwa sijui gundi hakuna. Mhe. Waziri, ningekuomba kidogo uende kutembelea kwenye ile sehemu ukakutane na wafanyakazi wa pale wakuambie zile changamoto zao, ili magari ya serikali yaweze kutengenezwa katika mitambo ile, naamini serikali itapata mapato mengi sana kama sehemu ile wataiangalia na kuipelekea vitendea kazi, kwa sababu serikali ina lengo la kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma zao kwenye serikali. Kwa hivyo, nakuomba sehemu hiyo uende kuiangalia.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije kwenye sehemu ya barabara. Mhe. Spika, kuna barabara ya Mgelema. Barabara hii imeshakua ni kilio kikubwa sana kwa watumiaji wa barabara ile. Mhe. Spika, Mgelema ni sehemu ambayo inatoa

karafuu nyingi sana, Mgelema inatoa karafuu ambazo zinatufanya sisi pia Waheshimiwa Wawakilishi tuliomo humu tupate maposho yetu na mishahara yetu kwa sababu tunategemea hizo karafuu, hawa watu wa Mgelema hawana ile nenda rudi ya kwenda kuuza magendo, ila wao karafuu zao zote wanapeleka Serikalini kwanza tuwapongeze. Lakini tunawatupa kwa sababu ile barabra tunakuta barabara nyingi sana zinatengenezwa lakini ile barabara iko vibaya, imechimbika, haijatengenezwa hata katika kiwango cha kutia kifusi.

Ningeiomba sana Wizara ya Mawasiliano iangalie ile barabara kwa sababu wananchi wake wanapata usumbufu sana, kutoa mzazi Mgelema kumleta njiani kwa ajili ya kwenda hospitali kuzaa hafiki kutokana na ubovu wa barabara ile, kwa hivyo, wanawake wanasumbuka na wanazaa kwenye magari kwa sababu barabara ni mbovu sana sana. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Wazir, aniambie ni lini barabara ile wataitengeneza japo katika kiwango cha kuweka kifusi.

Nije kwa Wizara ya Mawasiliano Pemba Mhe. Waziri, Wizara nyingi zilipokuja hapa zimeleta takwimu ya wafanyakazi ambao wamepelekwa katika masomo, lakini katika hotuba yako hii sijaona ni wafanyakazi wangapi wamesomeshwa katika Wizara yako, utakapokuja kwenye majumuisho Mhe. Waziri, nakuomba uniletee takwimu ni wafanyakazi wangapi katika kipindi hichi cha fedha kilichopita umewasomesha Unguja na Pemba, na niwafanyakazi wangapi unategemea kuwasomesha katika kipindi hichi cha fedha Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, niende kwenye suala la meli yetu mpya, tulikuwa na kilio cha meli, *Alhamdullilahi* tumekipata, lakini sasa kama walivyosema wenyewe kwamba meli ile ina matatizo, tunakuta kwamba tunatumia pesa nyingi katika kusafirisha magari kupeleka Pemba, Serikali pesa zile mimi naamini kwamba na wao pia wanazitaka, unatoa laki tano unasafirisha gari kwenda Pemba, mimi naamini kwamba ile meli yetu mpya nzuri ambayo wanasema kwamba wameisusia lakini si kweli, ila wanaipenda. Tutakapoifanyia marekebisho ule mlango zile laki tano tano naamini zikiingia kwenye Serikali, Serikali itafika pahali ambapo tunapategemea.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme mengi kwa sababu hii ni Wizara yangu na leo kidogo kifua changu kina matatizo tatizo, mimi naunga mkono hotuba hii asilimia sabini na thalathini nitaziingiza pale Mhe. Waziri, atakapokuja na hayo ambayo nimemuomba. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uhai, lakini pia nikushukuru wewe kwa kuweza

kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Wizara hii ya Mawasiliano na Miundombinu na Usafirishaji, Mhe. Spika, kabla ya kuchangia mchango wangu, nina michango kama mitatu tu hivi ambayo nafikiri itakidhi haja na muda kwa wakati wako.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, pamoja na Naibu Waziri wa Wizara husika pamoja na watendaji wake wote kwa namna wanavyosimamia na kutekeleza kazi zao katika Wizara yao hii kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa, pia, nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sijamshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Makamo Mwenyekiti ambaye amewasilisha hotuba hii kaka yangu Suleiman Sarahan Said maarufu 'Jembe', kwa kweli *style* aliyoitumia ningewaomba basi na wenzake kupitia kamati nyengine waige mfano wake katika kukamilisha kazi zao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mchango wangu uko katika maeneo matatu kama nilivyosema, eneo la kwanza ni eneo la bandari, nilipongeze Shirika kwa jitihada wanazozifanya katika kazi zao za kila siku katika eneo hili, mimi hapa nina kilio kidogo tu, nina kilio katika masuala mazima ya uwekaji wa makontena katika bandari na Wizara itakuja kunielezea mipango yake, kwa sababu jambo hili limekuwa linaleta usumbufu katika maeneo mbali mbali, katika usalama wa wafanyakazi kwa sababu kontena zinakwenda juu sana, ni hatari, lakini pia katika suala la uingizaji wa mapato kwa nchi yetu.

Kwa sababu imepelekea sasa hivi meli nyingi zinapokuja kwa wakati mmoja zinakuwa zinapata matatizo ya kuegesha katika bandari yetu kutokana na ufinyu wa eneo. Sasa mimi ninakuwa napata tabu kwa sababu tulizoea kuweka makontena Bwawani, Bwawani sasa hivi kama tunavyofahamu imechukuliwa na muwekezaji.

Sasa ningeiomba Wizara itwambie mipango yake kwa sababu najua tuna maeneo mengi ambayo ni ya wazi; tuna eneo la Maruhubi, tuna maeneo ya Tunguu, sasa inakuwaje kuwaje tunashindwa kutafuta eneo kuweza kufanya ile kazi ya kuweka makontena baadae tunatoa usumbufu kwa wafanyabiashara kwa mashirika ambayo yanakuja na meli zao kuwapa usumbufu wa kukaa kwa muda mrefu katika bandari yetu nje ya bandari.

Lakini pia tuna eneo ndani ya bandari maeneo ya kule kunakouzwa madagaa, kulikuwa kuna mabanda sasa hivi mabanda yamebomoka, yaani baada ya kuyatengeneza tumewapa watu sasa hivi wanauza mkaa na kuni, sasa hili kwa kweli linakuwa linatusikitisha sana. Kwa sababu hatuoni mipango mizuri ya Shirika katika kuweza kutatua tatizo hili tatizo ambalo lina muda mrefu. Sasa

Mhe. Wazir, atakapokuja atajitahidi kunipa maelezo ya kina ili kuona kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Jengine Mhe. Spika, nataka kuzungumzia katika suala la barabara za ndani na suala hili kwa kweli linakuwa linatupa kazi sana kwa sababu Sheria ya barabara ya ndani iko kwenye Serikali za mitaa, lakini najua kuna ushirikiano baina ya Serikali za mitaa na Serikali kuu kwa sababu Serikali za mitaa hawana zana na uwezo mdogo, lakini Serikali kuu kuna mfuko wa barabara na sasa hivi nashukuru kwamba mfuko wa barabara una mawasiliano mazuri na Serikali za mitaa, yaani Halmashauri za Manispaa katika kuona wanatunza barabara za ndani, niwapongeze kwa kuanza kutengeneza hizo barabara za ndani kwa kasi kabisa, tunajua tu barabara nyingi zimeanza kutengenezwa zikiwemo za Karibuni Jimbo la Kikwajuni zote zimefika asilimia kubwa, Jimbo langu la Kwahani nimepata barabara moja mpakani kutoka Muembeladu kwenda Mitiulaya.

Lakini kuna barabara kama mbili tatu za Jimbo la Fuoni nimeziona, mimi hapa Mhe. Spika, nilitaka Mhe. Waziri, atakapokuja anisaidie mfumo wanaotumia au vigezo wanavyotumia katika kuzijenga barabara za ndani, kwa nini niseme hivyo Mheshimiwa. Kwamba tunapata faraja ya kutengenezewa barabara zetu lakini tatizo yale maeneo ambayo yana tatizo kubwa ya kutengenezwa barabara za ndani hayatengenezwi, kwa sababu kuna maeneo hata ukisema ustahamili mwaka mmoja miaka miwili hayana tatizo.

Mhe. Spika, kuna maeneo ya jimbo kama la Pangawe, Jimbo la Fuoni, Jimbo la Welezo, Jimbo la Mtopepo barabara zake kama inanyesha mvua kunatokezea tatizo la kuweza kumkimbiza mgonjwa maeneo mengine gari hazipiti kabisa, yaani wananchi wa majimbo hayo wanakosa huduma ya usafiri nyakazi za mvua, sasa ninakuwa napata kigugumizi cha vigezo vinavyotumika kwa sababu maeneo mengine angalau yanaweza kuleta stahamala. (*Makofi*)

Kwa sababu sitegemei kwamba barabara zenye vishimo vidogo vidogo ukenda kuzitengeneza haraka, ukaacha barabara ambazo magari hayapiti kabisa, sasa nilitaka kujua vigezo ambavyo wanavyotumia katika kutengeneza hizi barabra za ndani, nimesema kwamba barabara zinatengenezwa, jitihada nzuri lakini tunachokikosea kuangalia ile *priority* ya maeneo ambayo yana matatizo sugu lakini tukenda maeneo ambayo matatizo yake yanaweza kustahamilika, sasa nataka kujua vile vigezo wanavyovitumia katika kuainisha barabara gani ambazo zitaanza mwanzo na barabara gani ambazo zitasubiri kidogo. Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho yake hapa atakuja kunisaidia huo utaratibu anaotumia.

Mhe. Spika, Pongezi, naomba sana nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Uwanja wa Ndege, tulikuwa tukipiga makelele sana kuhusu uwanja wa ndege, kila mtu alikuwa mkali, kaka yangu hapa mufti Shehe Jaku kama kawaida yake alipiga kelele sana na wengine wengi tu tulipiga kelele, lakini nataka nitoe pongezi kwamba tumeanza kuona mabadiliko uwanja wa ndege siku hadi siku. Na niwaombe kwamba jitihada zao zizidi kuendelea ili kuleta mandhari mazuri katika nchi yetu kwa wageni wetu ambao wanafika, kwa sababu tunajua kwamba mtu yeyote anapofika Zanzibar kama hakuja kwa meli akapita bandarini basi atakuja kwa ndege mwanzo aone eneo la Uwanja wa Ndege, sasa unapoingia katika nchi ukaona mazingira mazuri basi ni jambo la kuvutia sana, niwapongeze na niwaombe wazidishe jitihada kwa hili. (*Makofi*)

Nilisema michango yangu minne. La kumalizia Mhe. Spika, mimi niwaombe sana Mawaziri na watendaji wakati tunaingia katika baraza hili baadhi ya wananchi nje huko walikuwa wanasema kwamba hususan wafanyakazi kwamba, safari hii Baraza lainii, yaani wenyewe kwa wenyewe, lakini nataka niwaambie katika mwaka ambao wajumbe wataisimamia Serikali katika kuishauri, kuielekeza, kuikosoa na kuwafichua wabadhirifu na watendaji wasioitakia mema Serikali hii ya CCM basi ni Baraza hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nawaomba wajumbe wenzangu watumie nguvu zao za hoja kisheria, kikatiba na kanuni kuisimamia Serikali hii kuwaondosha wazembe, wezi na wazururaji katika serikali hii.(*Makofi*)

Mhe. Spika, tumeanza kwa maneno na baadhi ya Mawaziri wame-*take action* kwa maeneo yao katika kipindi kifupi sana, tuliwasifu hapa Mhe. Haji, hayupo namna tulivyokemea suala la ng'ombe tunachukuliwa mpaka majumbani sasa hivi ukiachilia wale wa barabarani, ni jambo zuri na jema na wengine nao wameanza kuchukua *actions,* Mhe. Waziri wa Habari, jitihada zake tunaziona. Sasa nataka kusema kwamba mabadiliko haya ya Mawaziri katika kukubali ushauri wa Wawakilishi, ushauri wa *back benchers* na wengine wafuate.(*Makofi*)

Sasa leo Mhe. Spika, natoa ujumbe kwa Wizara ya Miundombinu, lazima tuonee uchungu pesa za wananchi wanyonge wa nchi hii, kaka yangu Gavu hapa, mdogo wangu samahani, alikuwa anapiga kelele sana tunapolalamika kwa barabara; barabara zina gharama kubwa, barabara ya kilomita moja inatumia zaidi ya mamilioni ya pesa, kwa hivyo, tustahamili katika utengenezaji wa barabara. Lakini kinachonipa uchungu Serikali inatumia pesa nyingi tatizo la kutokutunza barabara zetu ambazo zinatumia gharama kubwa ya pesa za wananchi.

Mhe. Spika, kuna barabara tumeshaizungumza si chini ya vikao vitatu mpaka vinne huko nyuma, nasema Serikali hii ya awamu hii na Baraza hili tumekuja na kauli ya maneno na vitendo. Mhe. Waziri, aje aniambie barabara ya kwa Mchina kuelekea Mbuyu Mnene sababu ya kuruhusu kuwekwa magari katika barabara na kuimwagia *diesel* na kuondosha ubora wa barabara ile na kupelekea kutoa bughudha kwa watumiaji wa magari, yaani wa vipando pamoja na wanaotembea kwa miguu tatizo ni nini na lini ataiga mfano wa mawaziri wenzake kuondosha kadhia ile.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wa Kwahani, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nami nishukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa na vile vile, niungane na ndugu Mhe. Issa Ussi Haji (Gavu) na kwa jinsi ya umakini wako unavyoliendesha Baraza kwa umakini wa hali ya juu Mhe. Spika, nikupongeze kwa dhati kabisa.

Nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuona umakini wake kumteua Mhe. Ali Karume, kushika nafasi hii na vile vile, hakufanya kosa kumteua katibu wake katika Wizara hii, ni watu wenye uzoefu mkubwa kwa kiasi fulani, naamini wataweza, bila ya kusahau niwashukuru watu wa barabara *UUB.*

Mhe. Waziri, naomba unisikilize kwa makini hapa, watu wa *UUB* na Mfuko wa Barabara, watu hawa niwapongeze kwa dhati kutoka mwanzo mpaka mwisho katika mfuko wa barabara katika mazingira wanayofanya kazi nzito, mazingira wanayofanyia kazi wakiwa hawana vitendea kazi, vitendea kazi nafikiri tokea ukoloni mpaka leo vishachoka, haviridhishi na wanapata shida kubwa sana na sisi wengine huwa tunasaidia majimboni kwetu baada ya kuweka mafusi kwenye njia zilizokuwa hazipitiki. Lakini cha kusikitisha Mhe. Waziri, bajeti yao ni ndogo, tena ndogo mno, Mhe. Waziri, wewe ni msomi na nafikiri hoja zangu utazisikia, nafikiri utakaa na kuzipima na kuamua kwamba ninachozungumza sahihi si sahihi.

Hawa kwa kutegemea mfuko wa shilingi mia za mafuta hawezi kuendesha bajeti hii, lazima wafikiriwe, bajeti hiyo kila mwaka haizidi, ni pale pale, hata huyo mtoto akizaliwa hukua, hutambaa, akakweta, akapata mguu, akakamata kiwambaza, akaanguka mpaka akachanganya, bajeti hii uzoefu inaonyesha iko vile vile, tutaendelea kuwalaumu tu barabara mbovu, hatuwafanyi haki Mhe. Waziri, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, tena nafikiri

wanafanyakazi masaa ishirini na nne hawa watu. Lazima tuwafikirie, barabara zetu zimechoka, bajeti hii haikidhi ya shilingi mia, wanapata *resources* kwa njia moja tu, halafu hiyo hiyo Halmashauri wanaisubiri pesa hiyo wagawane, ni kitu cha ajabu, hatuelekei na hatuwafanyii haki kwa bajeti hii hatuwafanyii haki.

Lazima tuwaombee bajeti, kwa kutegemea mfuko huo haiwezekani kwa sababu Halmashauri pesa hiyo wanaisubiri kwenye mfuko huo, vitendea kazi hapa Mhe. Waziri, lazima hapa uje utueleze, vinginevyo, naomba isije ikajirudia historia tena ya Baraza hili dhidi yangu mimi, lazima tuwatetee ukweli utabakia kuwa ukweli, narudia tena nazungumza Kiswahili kungali mchana. Naomba historia isije ikarudia tena dhidi yangu bajeti...

Mhe. Spika: Mhe. Jaku, zungumza na Spika, usizungumze na Waziri tafadhali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, vyenginevyo, naomba historia isije ikazidi, lakini vyombo vile vina gharama kubwa, hakuna chombo cha milioni mia mbili, mia tatu mle cha kuanzia, watafanya kazi mazingira gani, spana mkononi siku zote, baada ya maelezo hayo bajeti hii hairidhishi hasa kwa mfuko wa barabara, na sisi Waheshimiwa, tumekuwa tukiwalaumu sana watu hawa barabara mbovu, barabara mbovu, watafanya nini wakati hawajawezeshwa, Mhe. Spika, nafikiri salamu hizo zimefika.

Jengine kidogo nije kwenye Sheria za leseni, askari polisi mtueleze nyie hii sheria imeshafutwa ya masaa 24, mtu anakamatwa anaambiwa apeleke leseni yake kufika kule anaambiwa masaa 24 zishapita, utaratibu gani huu? Kama imefutwa mtwambie sheria hii imefutwa kupeleka leseni masaa 24 kituo cha polisi, watu wanateseka hasa Tunguu na Dunga.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye rafiki zangu wa Mji Mkongwe wako juu huko, nazungumza hili kwa niaba ya wananchi na hapa nitahitaji maelezo ya kina kabisa Mhe. Spika, kufungwa kipande cha barabara ya Mkunazini hadi Skuli bado Serikali haijatoa *reason* ya kuwafahamisha wananchi, barabara ile kuna walemavu wana haki yao kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, kuna benki, kuna maskuli, kuna misikiti, kuna makanisa. Kipande kile kwenda kukifunga mtoto mlemavu tunamnyima haki yake, atafikaje skuli kule, miaka yote Mji Mkongwe upo kipande kile hakijafungwa, ndio kuongezeka kwa magari kweli, ni kitu cha kusikitisha. Narudia tena suala hili linanikosesha usingizi mimi.

Mhe. Spika, Kuna *garage*, leo kisingizio *UNESCO*, mtu yuko Uingereza, yuko Marekani anakuja kutupangia chakula chetu tule saa ngapi sisi! Inabidi

UNESCO ni muhimu kuliko wananchi hawa waliokuwepo hapa? Hii nchi au serikali narudia tena isingekuwepo madarakani bila ya kuwepo wananchi, barabara ile ifunguliwe, vyenginevyo, histori isije ikajirudia tena, nazungumza Kiswahili kinachofahamika.

Kuna walemavu wanakwenda skuli wakifika pale Polisi wanasimamisha magari hayendi, hatuwatendei haki chombo chao ndio hiki tuje kuwasemea, sio wende marikiti ukaseme maneno haya au sokoni Mwanakwerekwe, chombo chao hiki wapate kusikia kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Ibara 88. Watoto walemavu hawakuomba na mimi pengine Mwenyezi Mungu aje anipe ulemavu nisiotarajia, kwa sababu 'hujafa hujaumbika', watu wakenda skuli na gani wakifika pale wanasimamishwa, mtu kampakia kwenye vespa barabara kipande kile kimefungwa.

Mhe. Ali Salum, alizungumza tulipiga kelele sana suala la uwanja wa ndege kipindi kilichopita tukafika tukafanikiwa, Mkurugenzi akafahamu kweli uko vipi, kipande kile kifunguliwe isiwe sababu ya *UNESCO,* hii haiingii kichwani kabisa. Ninajua mimi *UNESCO* kabla ya kujiunga kwenda kule mnapeleka sheria za nchi yenu zinasemaje ndipo mnakubaliwa. *UNESCO* mambo ya majengo na kipande chengine kile cha barabara ya Malindi kwenda bandarini, kuna mgonjwa anapelekwa kwenye boti siku nyengine hawezi kupanda ndege wanateseka, chombo chao ndio hichi nimekuja kuwasemea. Wajibu wangu kusema utekelezaji utafutata baadae, lakini kipande kile cha Mkunazini, kipande cha Malindi wagonjwa kupelekwa kwenye maboti wateseke kule wachukuliwe kama mzega mzega aa, haifai.

Mhe. Waziri, nije kunako Shirika la Nyumba, nimshukuru sana baba yako Hayati Abeid Amani Karume, Mungu amlaze mahali pema, ndio nikasema Dkt. Shein hakukosea kukuba wizara hii na ndugu yako aliyemaliza Urais nimshukuru sana Mhe. Amani Abeid Karume, baba yako ndio aliyejenga nyumba za maendeleo nchi hii, akatangaza elimu bure, maji bure, matibabu bure. Lengo la kujengwa nyumba zile ni kuwasaidia wanyonge na zikalala zile nyumba akaja akamaliza sijui kama kaka yako au mdogo wako hapo sijui, ndio aliyekuja kumaliza nyumba namba tisa sijui namba 8. Nimshukuru sana na Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu na afya njema. Huo ndio ukweli baba yako alioufanya, nafikiri na wewe ndio utakuja kurithi, zile nyumba zimetupwa, lengo la zile nyumba ni kuwatatulia maskini kwa makaazi.

Nilisema mwaka jana tunaanzisha Shirika la Nyumba hatujawa tayari humu ndani, mimi niambiwe Shirika la Nyumba tokea kuanzishwa limefanya kitu gani kipya hapa. Leo kodi zile shilingi 50,000/- chumba unamuinua

mwananchi, si unakuja kumkandamiza, lengo lake nini, wanafaidika vipi matunda ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kitu cha kusikitisha wamepewa watu nyumba nyengine ziwasaidie wanalipishwa, haielekei, nyumba tokea alipojenga baba yako za Michezaji hata chokaa hazijatiwa mpaka hii leo. Hatuwezi kwenda, wananchi wanateseka tu, kipato chenyewe kiko wapi, mshahara laki tatu nyumba ile akalipe 150,000/, ana watoto atawalisha nini, atawavisha nini, wanataka matibabu na maji, maji yenyewe hayatoki. Nitatofautiana na Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Soud, jana alisema hapa maji kila kona yanatoka, yako wapi? Hatuwezi kwenda. Kwa hivyo, Mamlaka ya Mji Mkongwe vile vile.

Baada ya hapo, nije jumba la *train* la marikini. Kwa masikitiko makubwa sana mwezi huu mtukufu huu wa Ramadhani na hapa nitahitaji maelezo vile vile, wananchi waliomba kwenye serikali yao wapewe muda angalau Ramadhani iishe ili wafanye biashara zao mali zisije zika-*expire*, wana watoto na familia zao. Lakini cha kusikitisha kibali nije nioneshwe mimi kama kiko tayari cha ujenzi wa nyumba ile, kama kiko tayari. Michoro haijawa tayari, halafu ile michoro baada kuchorwa ipelekwe *UNESCO* ikapasishwe, kitu cha ajabu tunawakandamiza wananchi.

Mchoro uchorwe na upelekwe *UNESCO* tukaombe *hewalla* bwana tusaidieni mchoro upasishwe ili tukajenge nyumba ile, nije nioneshwe vitu, kibali, michoro, halafu tenda haijatangazwa nyumba ile, mtakuja mtatueleza.

Mheshimiwa, kwa kumalizia haraka haraka nije katika Shrika la Bandari, Shirika la Bandari limeoza na linaendelea kuoza na serikali imefika pahali tayari ilibinafsishe lile Shirika. Miaka yote tunadanganywa hata katika hotuba za Mhe. Rais, mara ngapi huwa inadanganywa katika vitabu hivi, hakuna ukweli. Vitendea kazi bandarini siku zote viko njiani, vinakuja, sijui njia iko wapi, kama *no entry*, hiyo haifiki, vitendea kazi havipo. Watu wanateseka na meli, meli sasa hivi huku Zanzibar hazitaki kuja huku Mhe. Spika. Meli zimekaa Chumbe karibu sita nimekwenda kuziangalia Mhe. Raza, anajua. Sasa haya mapato tutayapata wapi? Ng'ombe ukampa malisho mazuri ndio utategemea kukamua maziwa mengi. Sio kuwa tunapiga kelele tu kwa mdomo, vitendo havipo *we are not serious*. Makontena kule ni mengi, kuna tende, bidhaa sasa hivi hazijulikani na mwezi wenyewe ndio huu zinataka kushushwa, vitendea kazi vikakodiwe nje.

Shirika lishafika tayari wala tusione haya tubinafsishe tu, serikali ninafikiri itapata mapato zaidi, ukafanya kazi hiari yako mwenyewe kama huwezi utaona hapa nitegee hapa nifanye hivi, lakini serikali iingie ubia.Tumeshuhudia kule

Bara *TICTS* imekabidhiwa inashusha makontena, tujaribu kuiga, vyenginevyo, hatuwezi kufika Mhe. Spika.

Kwa kumalizia kuhusu kituo cha daladala, hizi kelele nimezipiga muda mrefu sana. Mhe. Zulfa, kazungumza hapa, kweli tuna imani na wananchi wetu mpaka leo nishaahidiwa katika chombo hichi kituo hichi kitajengwa, kitajengwa na miaka mengine itakwenda zake. Kuna kituo cha daladala pale *traffic light* tunaambiwa kitasogezwa mbele au sijui kitarudi nyuma au kitakuwa katikati mpaka leo.

Tuangalie Darajani pale, Kauli ya Serikali imetoa kituo cha Mwanakwerekwe kitasogezwa mbele, sijui mbele ya wapi kimesogezwa karibu uwanja wa ndege au wapi, sijui, chombo ndio hichi cha wananchi. Na kwa mujibu wa Katiba, Mhe. Spika, naomba ninukuu Ibara ya 88(a), inasema;

> "Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na kifungu cha Katiba hii litafanya kazi kwa mambo yafuatayo...".Kazi za Baraza Mheshimiwa. "...kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria",(b) "Kujadili shughuli za kila wizara wakati wa kila kikao cha mwaka bajeti katika Baraza la Wawakilishi...".Ndio majukumu yetu Waheshimiwa Wajumbe, hao, Kanuni ya Zanzibar hiyo.(c)"Kuuliza maswali mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi".(d)"Kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika nchi ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa".

Kwa mujibu wa Katiba tuliyopewa na si maneno yangu hayo. Leo wananchi wanaotoka Pemba wakafika Unguja kituo cha gari hawakijui wakapande wapi. Mtu ana watoto wawili na mkungu wa ndizi na kuku katia kwapani. Huu ndio wajibu wetu kuja kusimamia na kuihoji serikali.

Mhe. Spika, naona ushawasha taa yako, sitounga mkono bajeti hii mpaka nitakapopata maelezo ya kina.Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hii siku tukufu ya Ijumaa kuja hapa kuendelea na kikao chetu.

Mhe. Spika, pia, naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Ali Karume, kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na

Usafirishaji, hongera sana Mhe. Waziri. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri Mhe. Mohammed Ahmada na Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Mustafa Aboud Jumbe.

Mhe. Spika, timu hii ya watu watatu hawa viongozi wa wizara hii nahisi itatuletea maendeleo sana katika wizara hii, hongereni sana. Kwa sababu muda umeenda sana Mhe. Spika, mimi nitachangia mambo kidogo lakini kwa uharaka kidogo na zaidi nitachangia katika miradi ya maendeleo, miradi ya barabara, bandari mpya ya mpiga duri, halkadhalika na shughuli nyengine za uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, kwa upande wa barabara, kwanza niwapongeze sana Wizara na Idara yetu ya *UUB* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kama walivyotangulia Waheshimiwa Wajumbe wengine kazi za ujenzi wa barabara zina gharama kubwa sana, bahati nzuri na wewe ushawahi kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hivyo, unazijua vizuri. Ni gharama kubwa lakini humu katika bajeti yetu hii ipo mipango ya kuziendeleza barabara za Wete/Chake, Bububu/Mkokotoni na baadhi ya miradi mengine mikubwa.

Ningeliiomba Serikali kupitia wizara hii kufanya juhudi kubwa kumaliza barabara ya Wete/Chake. Ninafikiri sasa karibu miaka 7 tangu mradi ule umeanza ujenzi ni hatua nzuri iliofikia maana yake barabara ya Wete/Konde tayari imemalizika na Wete/Gando tayari imemalizika. Kwa hivyo, tunahitaji na Wete/Chake nayo imalizike.

Lakini kwa upande wa Unguja barabara ya Bububu/Mkokotoni ni muhimu sana, barabara ile imejengwa muda mrefu ina matatizo mengi, barabara nyembamba na haiko katika kiwango. Tunatarajia kwa mujibu wa mpango wa serikali kwamba, barabara ile itaanza pale Kwanyanya mpaka Mkokotoni. Ni matarajio yangu kwamba wakati wa ujenzi huu hatua za fidia kwa wananchi zitachukuliwa mapema kulipwa ili kusiwe na mgogoro, lakini pia tutakuwa na barabara nzuri ya kileo.

Mhe. Spika, pia, zipo baadhi ya barabara ambazo nawaomba Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wasishughulikie kwa uzuri zaidi. Ipo barabara ya Matemwe/Muyuni, hii barabara ni changamoto ya muda mrefu na zaidi kwa Chama chetu cha Mapinduzi. Tumekuwa tukiieleza kwenye ilani karibu miaka 10 na bado barabara hii haijajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, aichukulie kwa kipaumbele sawa sawa na barabara ya pale Kiongele. Barabara hii imetajwa kwa muda mrefu na barabara ya

Donge kwendea Muanda. Mhe. Spika, hizi ni barabara ambazo zimetajwa kwa muda mrefu.

Lakini pia Mhe. Spika, katika ziara za marais kuanzia Mhe. Aman na Mhe. Dkt. Shein walivyotembelea walizungumzia ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mwakaje, Mwachealale mpaka Bumbwisudi.Tunaomba hiyo ahadi ya serikali itekelezwe na barabara ya Kama meli kumi mpaka kwenye vikosi vyetu vya KMKM na JKU na barabara ya Kihinani hizi ziko katika ahadi za Rais, kwa hivyo, naomba hizi zifanyiwe majibu yake haraka haraka.

Lakini niungane na Mhe. Jaku, kwamba ipo haja kwa serikali na bahati mbaya kwamba watu pengine wanafikiria mfuko wa barabara uko wizara hii lakini mfuko wa barabara uko Wizara ya Fedha. Niombe basi kupitia mfuko wa barabara kuwe na mpango maalum wa serikali kuisaidia Wizara ya Mawasiliano kupitia Idara ya *UUB* kuwa na mpango wa kununua vifaa kupitia mfuko ule wa barabara, sio kujenga na kutengeneza barabara tu. Kuna umuhimu pia wa kuwa na vifaa kwa sababu Idara yetu ina wataalam, wafanyakazi wana juhudi lakini vifaa vyao ni vibovu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aliangalie hili.

Mhe. Spika, jengine ni huu mradi wa bandari ya Mpigaduri, hili ni jambo ambalo litaleta faraja kubwa kwa Zanzibar. Sasa hivi lipo tatizo la makontena kutoka Dar-es-Salaam kuja Zanzibar kukaa muda mrefu, mengine yanakaa miezi 3, miezi 6 mpaka bidhaa zinaoza. Ninafikiri tukiweza kujenga bandari ya Mpigaduri tutaondoa tatizo la msongamano wa makontena na hili lililozungumzwa kuhusu makontena yawekwe wapi, suluhisho lake ni ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Kwa hivyo, ninafikiria kwamba serikali inafanya jambo zuri na inaendelea vizuri.

Mwisho, Mhe. Spika, nizungumzie Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa viwanja hivi, ameleta mageuzi makubwa ya uwanja. Sisi ambao tuliwahi kuongoza pale tunajua kwamba Mkurugenzi huyu amefanya kazi kubwa. Niombe, kuna mambo kama mawili.

Kwanza, naomba sana wakati umefika na zaidi tukifungua jengo letu jipya la *Airport* lazima tuimarishe usalama. Kwa dunia ya leo Viwanja vya Ndege vya Kimataifa shughuli za usalama katika viwanja zinafanywa na makampuni binafsi. Inawezekana serikali ikaangalia kama itaingia *PPP* ama vipi, lakini kuna mashirika ya ndege lazima watakuuliza kiwanja chenu kinalindwa na nani ili waweze kuleta ndege zao. Sasa hili ni jambo jema hatuwezi kuwa na uwanja mzuri, majengo mazuri, kwa sababu uwanja ule sasa ni mzuri sana, *run way*

nzuri, *tax way* nzuri, kila sehemu pale majengo yenyewe mazuri, kwa hivyo, lazima kuwe na usalama mzuri.

Lakini ninamuomba Mhe. Waziri, katika kulinda maslahi ya nchi aiangalie bodi yake, kwa sababu tunasikia maneno baadhi ya wajumbe wao wamo mule ambao hawaitambui hata serikali yenyewe, sasa mtu anakuwaje kwenye bodi mtu ambaye haitambui serikali. Naomba Mhe. Waziri, uchukue nafasi uwachomoe wale ambao hawaiungi mkono serikali au hawaitambui na watoke kwenye bodi. Haiwezekani mtu unatukana na asubuhi unaingia katika nyumba hiyo hiyo.Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, Bodi ya *ZAA*, Mkurugenzi mzuri lakini bodi yake lazima imurikwe, je, wote ndio au wengine wana mazonge mazonge.*(Makofi)*

La mwisho, ni kwamba nikutakie kheri kuna kipindi mimi nilikuwa waziri hapa siku moja ilizama meli nilikuwa Mwanza, wakafa watu sita ilizama bandarini kabisa. Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi akasema waziri ajiuzulu kwa kuzama meli na kufariki watu 6, lakini sikujiuzulu. Bahati nzuri kwenye awamu nyengine akawa Waziri wa Mawasiliano yeye, hatua ya mwanzo walikufa watu mia moja na kitu, lakini mara ya pili wakafa watu karibu 300 chini ya mikono yake, hatimae ilibidi ajiuzulu kwa sababu watu walikuwa ni wengi.

Sasa huwezi kuwa binaadamu ukawa unamuombea mwenzako mabaya, tunataka Mhe. Waziri ufanye vizuri na Naibu Waziri afanye kazi vizuri, Katibu Mkuu na watendaji wake wafanye kazi vizuri. Tuna matumaini makubwa, hii Mhe. Spika, wizara hii si ya maneno, wizara hii ni ya kufanya vitendo vikaonekana, ujenge barabara safi, ujenge bandari safi, uwe na viwanja vya ndege safi, hapo utakuwa umetimiza wajibu wako. Kwa bahati nzuri umeongezewa na nyumba, nyumba zenyewe mbovu, kwa hivyo, bado pia una kazi kubwa huko, Mhe. Waziri, nakuombea heri, ahsante sana naunga mkono asilimia mia bajeti hii.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said, Waheshimiwa wajumbe, muda tulionao hauruhusu tena mchangiaji mwengine kuchangia. Orodha yetu mpaka sasa hivi ishavuta mpaka watu 38, kwa hivyo, nilikuwa ninakuombeni waheshimiwa ili wapate wengi basi mturuhusu kesho pia maswali tusiyaweke ili waweze kupata kuchangia walio wengi. Sina haja ya kutoa hoja ili kuondosha maswali, Spika, ana uwezo tu wa kuamua kwamba yasije, kwa hivyo, kesho nitatoa maagizo kwamba yasije yale maswali ili muweze mtakapokuja saa 3.00 waanze kuchangia moja kwa moja.

Baada ya maelezo hayo ninaahirisha shughuli za Baraza mpaka kesho siku ya Jumamosi saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 9.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 18/06/2016 saa 3.00 asubuhi)